Jumamosi Desemba 21, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581897 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital 0677 020 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2

**Wajeruhiwa** kwa mafuta petroli yaliyohifadhiwa ndani ya duka



UKURASA WA 5

**NSSF** kujenga hoteli yenye hadhi ya nyota tano Dodoma



UKURASA WA 7

**Mhudumu** baa aachiwa huru kesi ya dawa za kulevya



RIPOTI MAALUMU

# Taharuki wanafunzi na wazazi shule kufungwa

UKURASA 4 & 7




Shule inayodaiwa kufungwa

UKURASA WA 17

## RAIS TSHISEKEDI AMFUTA KAZI MKUU WA MAJESHI

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amemwondoa madarakani mkuu wa majeshi na maofisa wengine wa kijeshi...



## Wanaume hatarini kuathirika tatizo la afya ya akili, sababu zatajwa

UKURASA 3

## RC Mtaka ageuka mbogo kukithiri kwa mauaji, ukatili

• **Ahoji** chanzo kama ni tatizo afya ya akili au ushetani... *Ukurasa 2*



**MICHEZO** MPANZU KUIPAISHA SIMBA KAGERA LEO? UK.24 **MAONI,** UK.6

# Chongolo awapasha viongozi, wanasiasa

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

VIONGOZI wa kisiasa na serikali mkoani hapa wametakiwa kutafsiri dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025-2050 kwa manufaa ya wananchi.

Wito huo ulitolewa juzi na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, wakati wa hafla ya uzinduzi wa hamasa ya uandikishwaji katika daftari la mpigakura Wilaya ya Njombe.

Chongolo alisema moja ya kosa ambalo limewahi kufanyika ni kutoitafsiri dira hiyo kutokana na changamoto za Mkoa wa Njombe.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kujipanga kutafsiri dira hiyo kwa kuihusisha na namna ambavyo mkoa huo unaweza kunufaika na fursa za kiuchumi kutokana na kuwa lango la kimataifa la biashara kwa kuwa nchi nyingi zilipitisha mizigo hasa Makambako.

"Sasa hivi tuna dira mpya ambayo inaanza mwaka kesho, itaenda kwa miaka 25 tujipange kuitafsiri kwa sura hiyo, Njombe hili ni lango la mikoa mingi, na ni lango la mataifa, hakuna mzigo unaotoka Zambia bila ya kupita hapa," alisema Chongolo.

Aliwataka viongozi hao kuachana na tabia ya ubinafsi kwa kuwawezesha vijana kupata fursa za kiuchumi ili kukuza kipato chao.

Awali Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama hicho Wilaya ya Njombe, Erick Ngole, aliwataka vijana kuhamasisha wananchi kushiriki katika uboreshaji wa daftari la kudumu la mpigakura ili wapate sifa ya kushiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.



Aliyekuwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Huduma ya Mabasi yaendayo kwa haraka (UDART), Robert Kisena, akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana, kusikiliza mashataka yanayomkabili ya uhujumu uchumi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# RC ageuka mbogo kukithiri mauaji, ukatili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amekuja juu na kuhoji kukithiri kwa matukio ya mauaji, ukatili wanawake na watoto mkoani hapa kama ni matatizo ya afya ya akili au ushetani.

Mtaka alitoa kauli hiyo kwenye kikao na makundi mbalimbali kichofanyika mjini hapa juzi kujadili jinsi ya kukabiliana na matukio hayo katika jamii.

Ni baada ya kueleza kuchukukizwa kwake na kukithiri kwa matukio hayo na kuchafua sifa ya mkoa huo.

Alisema matukio hayo yanaondoa ubinadamu na kufedhehesha utu wa mtu na haki katika jamii, hivyo hayavumiliki na hayapaswi kuendelea kutokea mkoani hapa.

"Kwa kweli ni matukio ambayo binafsi yamenifedhehesha sana, yamenisikitisha sana, tunataka kujenga jamii ipi, huu utamaduni unatoka wapi?" alihoji Mtaka.

"Nadhani serikali tumezungumza hili jambo kijuu juu sio kwenye uzito ambao unafanana na hiki kinachotokea hizi siku za karibuni, mtaona huko mitandaoni matukio kila unaposoma unajiuliza yanafanywa na binadamu kabisa mwenye akili timamu," alisema.

Mataka alisema tofauti na mikoa mingine nchini kamanda wa polisi anashughulika na matukio ya uhalifu, lakini kwa Njombe mengi yanafanywa ndani ya familia.

"Sasa imekuwa kazi ya Jeshi la Polisi kuripoti leo kuna kituko hiki, ni matukio ambayo yapo nje ya uwezo wa kusema Polisi wameshindwa kufanya kazi yao," alisema.

Mtaka alisema jamii na kila mmoja kwenye nafasi yake ya uongozi au mazingira, anapaswa kuzungumza kwa uzito mkubwa.

"Hatuwezi kuwa na mkoa ambao ukiamka unaona mitandaoni mwanamke kakata mwanaume sehemu za siri sasa hapo RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) anahusikaje? Mara kuna mwanaume ameingiza mkono kwenye maumbile ya nyuma ya mwanamke katoa utumbo, sasa hapo polisi anahusikaje," alisema.

Alisema kama tatizo ni afya ya akili, viongozi wa dini wanapaswa kuhubiri katika nyumba za ibada kuhimiza waumini wao wakapimwe na kupatiwa ushauri wa kisaikolojia.

"Viongozi wa siasa, sasa tuzungumze, tujiseme, tusemane, unasoma mitandao mpaka unashangaa sisi mkoa tumepata shida gani, " alisema Mtaka.

Hata hivyo, alisema historia ya mkoa huo, matukio ya visa mara watoto wamefanya hivi mara vile, wakati wengine huoni ushirikina bali unaona ushetani, alisema Mtaka.

Akitoa takwimu za matukiao hayo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahmoud Banga, alisema kuanzia mwaka 2021 hadi Desemba mwaka huu, matukio 279 ya mauaji yaliripotiwa katika vituo vya jeshi hilo.

Kwa mujibu wa Banga, ukatili wa kijinsia kwa ubakaji zaidi ya 820 yaliripotiwa.

Alisema kwa makosa ya ulawiti 91 yaliripotiwa, watoto wadogo kuanzia miaka mitatu hadi 17 ndio waathirika na kwa watu wazima kuanzia miaka 18 na kuendelea.

Kamanda Banga alisema uchunguzi wao umebaini kuwa wanaolawitiwa ni watoto wadogo kati ya miaka mitatu hadi miaka 17 ndani ya familia na kufanywa siri.

"Kuongezeka kwa matukio hayo ni kutokana na kuzidi kuelimisha jamii na watu wanajitokeza vituo vya polisi kutoa taarifa," alisema.

Kuhusu mauaji, Banga alisema ni kutokana na imani za kishirikina, migogoro ya ardhi, familia na wivu wa mapenzi. Mmoja wa wakazi mkoani Njombe, Joram Hongoli, alisema kukithiri kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto kutokana na wazazi na walezi kujiondoa katika jukumu la malezi na kuwaacha wakizagaa mitaani bila uangalizi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Wajeruhiwa na mafuta petroli yaliyohifadhiwa ndani ya duka

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

WATU wanane wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi iliyoko Mjini Vwawa, baada ya kujeruhiwa katika ajali ya moto baada ya duka la kuhifadhi na kuuza vinywaji vya jumla na rejareja (depo) kuwaka moto.

Inadaiwa kuwa moto huo umesababishwa na mafuta ya petroli yaliyohifadhiwa ndani ya duka hilo.

Ajali hiyo ilitokea juzi katika kijiji cha Ihowa, Kata ya Luanda, wilayani Mbozi, kwenye nyumba ambayo pia hutumika kama duka la kuuza vinywaji vya jumla na rejareja.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ihowa, Spidi Mbembela, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kudai kuwa, majeruhi wengi wa ajali hiyo ni wale waliofika eneo la tukio kwa lengo la uokoaji.

Alisema chanzo cha ajali hiyo kinadaiwa ni baada ya kulipuka kwa dumu la mafuta ya petroli ambalo lilikuwa limehifadhiwa ndani wakati mama mwenye nyumba hiyo, Rose Patrick, akiaanda chakula ndani ya duka hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari, mganga aliyekuwa zamu katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi, Dk. John Mwanyingili, alikiri kupokea majeruhi hao wanane juzi saa 12:00 jioni, ambao wamefanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu.

Dk. Mwamyingili alisema majeruhi hao ni pamoja na Rose mwenyewe na wengine ni Isambi Mwene (34), Maneno Jullius (49), Fadhiri Festo (32), Lewis Patrick (19), Frank Msyan (40) na Matokeo Islam (51).

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Wanaume hatarini kuathirika afya ya akili, sababu zatajwa

**Na Grace Mwakalinga**

WANAUME wako katika hatari kubwa ya kuathirika zaidi na changamoto ya afya ya akili ndani ya miaka mitano hadi 10, kutokana na tabia zao za kuwa wasiri katika kuyashughulikia matatizo yao.

Katika mahojiano maalum na Nipashe, Mkurugenzi wa Taasisi ya Empower Youth Prosperity (EYP), Ipyana Mwakyusa, alisema hali hiyo inatarajiwa kuongezeka ndani ya kipindi hicho, ikiwa tatizo hilo halitashughulikiwa mapema.

Akizungumzia changamoto zinazowakumba wanaume, Mwakyusa alisema utafiti uliofanywa na taasisi hiyo umebaini kuwa watu wa kundi hilo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazochangia kufanya uamuzi mgumu unaoathiri maisha yao.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo, EYP ilianzisha jukwaa la Men's Conference miaka minane iliyopita kwa ajili ya kuwawezesha wanaume na wavulana kutoka maeneo tofauti, hususan Mkoa wa Mbeya, kujadili changamoto wanazopitia na kupata suluhisho kwa kushirikiana.

"Mpaka sasa, zaidi ya wanaume 500 wamepata fursa ya kushiriki na kujadili changamoto zao kupitia jukwaa hili, jambo ambalo limewasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na msongo wa mawazo," alisema Mwakyusa.

Alisema tatizo la akili kwa wanaume bado lipo juu hasa kutokana na usiri unaowazunguka katika kushughulikia matatizo yao.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2023, wanawake wanaongoza kwa kufanya majaribio ya kujiua au kujidhuru lakini mara nyingi hawafanikiwi katika azma hiyo.

Ripoti hiyo inaonesha pia kila siku wasichana 140 wanauawa na watu wa karibu, huku takwimu zikionesha kuwa wanawake 8,500 wanauawa kila mwaka duniani kote.

Aidha, ripoti hiyo inabainisha zaidi kuwa wanaume ndio wahusika wakuu wa mauaji hayo na wengi wao wanakumbwa na changamoto za afya ya akili.

Kutokana na hali hiyo, EYP imesisitiza umuhimu wa jamii kuzungumzia masuala ya afya ya akili kwa uwazi, hasa kwa wanaume na kutafuta njia bora za kushughulikia changamoto hizi.

Mwakyusa alitoa wito kwa serikali kuweka mazingira rafiki kwa wanaume ili waweze kujadili matatizo yao bila hofu na kupata msaada wa kitaalamu. "Tunahitaji juhudi za pamoja kuondoa unyanyapaa unaowazuia wanaume kuzungumza masuala yao. Ndani ya miaka mitano hadi 10, wanaume watakuwa hatarini zaidi kama hatua za haraka hazitachukuliwa," alisisitiza Mwakyusa.

EYP inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuhusu afya ya akili kwa lengo la kupunguza majanga yanayotokana na changamoto hizo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (SFD), Sultan Al-Marshad, baada ya kufanya mazungumzo kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kati ya mfuko huo na Tanzania, akiwa na mawaziri wenzake wa kisekta, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum (hawapo pichani), yaliyofanyika makao makuu ya mfuko huo, Mjini Riyadh, Saudi Arabia, jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Rais aanika sababu kujenga nyumba waathirika Hanang

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema uamuzi wa kujenga nyumba 109 kwa waathirika wa maafa ya maporomoko ya tope Hanang mkoani Manyara, umelenga kuwasaidia wananchi kurejea katika hali zao za kawaida.

Katika ukurasa wake wa Instagram jana, Rais Samia aliweka picha mbalimbali za nyumba hizo na kuandika maneno yanayosema: "Baada ya kazi nzuri kwa kipindi cha mwaka mzima, leo (jana) tumekabidhi rasmi nyumba 109 kwa ndugu zetu walioathiriwa na maporomoko ya tope mwezi Desemba, mwaka jana, wilayani Hanang mkoani Manyara.

"Uamuzi wa kujenga nyumba hizi umelenga kuwasaidia ndugu zetu hawa kurejea katika hali yao ya kawaida ya maisha baada ya changamoto ile ambapo baadhi walipoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine kupoteza kila walichokuwa nacho," aliandika Rais Samia.

Akizindua nyumba hizo jana zilizojengwa katika Kitongoji cha Waret, wilayani humo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwaeleza wananchi kwamba Rais Samia anawapa pole waathirika wote na amesisitiza kuwa serikali itawasaidia ili waendelee na maisha yao kama ilivyokuwa awali.

Alisema ujenzi wa nyumba 73 kati ya 109 umegharamiwa na serikali kuu na kujengwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA-JKT); nyumba nyingine 35 zimejengwa na Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania, ilhali nyumba moja imejengwa na Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) .

"Kutokana na maafa hayo, nyumba 109 zilihitaji kujengwa upya kwa haraka, hivyo kwa kuzingatia athari hizo na kwa upendo wake, Mheshimiwa Rais Samia alitoa maelekezo ya kujenga nyumba bora na za kudumu katika eneo salama kwa waathirika waliopoteza makazi yao.

"Ujenzi huu ni ishara ya kujali, upendo na dhamira ya serikali ya kuendelea kuwa pamoja na wananchi wakati wa shida," alisema.

Majaliwa alisema Rais Samia alitoa Sh. bilioni 1.38 kwa ajili ya kuweka huduma za kijamii ikiwamo umeme, maji na barabara za uhakika; lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa kila nyumba inafikiwa na huduma hizo.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu aliwaagiza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang waratibu mchakato wa ugawaji wa viwanja vya ziada vilivyoko katika eneo hilo ili kuliendeleza.

"Tunataka eneo hili lisitambuliwe kama makazi ya waathirika, bali kijiji rasmi chenye huduma zote muhimu za kijamii na liwe kielelezo cha maboresho ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wote," alisema.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi, alimshukuru Rais Samia kwa miongozo, maono na fikra thabiti ya namna ya kukabiliana na kurejesha hali wakati yalipotokea maporoko ya tope hilo.

'Ujenzi wa nyumba hizi ni maono yake, pia ameleta majiko ya gesi 109 ambayo watakabidhiwa wakazi wa eneo hili," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Msalaba Mwekundu, Lucia Sebastian, alisema ujenzi wa nyumba 35 uliofanywa na taasisi hiyo unaashiria umoja ambao unawatambulisha kama Watanzania.

"Kwa pamoja, tumetoa makazi; tumetoa amani na usalama kwa familia hizi na tumejenga maisha yao upya. Ushiriki wa TRCS katika safari hii umeongozwa na dhamira yetu ya kusaidia jamii wakati wa shida na dharura," alisisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine waliokabidhiwa nyumba, Kizito Joachim, alimshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa aliyoifanya tangu kutokea kwa janga hilo mpaka sasa wanapokabidhiwa nyumba hizo.

"Tunakumbuka upendo wa Rais Samia; hakika alikuwa mfariji mkuu na tunaendelea kumwombea kwa Mungu. Kwako pia, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru wewe kwa kuzielekeza wizara na wadau mbalimbali kuja kutunusuru kutokana na janga lile," alisema.

# Magari 10 yatolewa kukoleza kampeni Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imetoa magari 10 kwa ajili ya Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ili kuongeza kasi ya utoaji huduma hiyo sambamba na elimu ya sheria na katiba kwa Watanzania.

Akizungumza jana jijini hapa katika hafla ya kukabidhi magari hayo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema kupitia vitendea kazi hivyo, kampeni itafikia mikoa sita kwa wakati mmoja.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa namna anavyotuwezesha kutekeleza programu zetu mbalimbali. Kampeni hii hadi sasa imefikia mikoa 11, tumebaini njaa na kiu ya haki kwa Watanzania ni kubwa sana, hivyo vilihitajika vitendea kazi mbalimbali yakiwamo magari.

"Magari hayo dhumuni lake ni kusaidia watendaji wa wizara pamoja na wadau wengine wanaoshirikiana nao katika kampeni hii ili kuwafikia Watanzania kona zote za Tanzania na kukidhi kiu yao ya kupata haki, elimu ya sheria na katiba," alisema.

Dk. Ndumbaro alitoa rai kwa madereva kutunza vizuri magari hayo ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

"Tuna kila sababu Katibu Mkuu na watendaji wako katika kampeni hii kufanywa mikoa sita kwa wakati mmoja, awali tulikuwa hatuwezi kwasababu ya vitendea kazi," alisema.

Alisema katika maeneo ambayo yamefikiwa na kampeni hiyo wameona kuna uhitaji wa kurudi tena hasa migogoro ya wakulima na wafugaji na vizuizini yaani kwenye magereza.

Waziri Ndumbaro alisema hadi sasa kampeni hiyo imeshafikia mikoa ya Morogoro, Manyara, Singida, Mara, Simiyu, Ruvuma, Shinyanga, Iringa, Songwe, Dodoma na Njombe.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Eliakim Maswi, alisema magari hayo yamenunuliwa kwa fedha za serikali kwa ajili ya kazi maalumu.

Maswi alisema yatasaidia pia, watumishi wa wizara hiyo kutekeleza majukumu yao ya kawaida na kutoa msaada wa kisheria.

"Mabasi haya mawili yatatumika kubeba watumishi katika shughuli za kampeni tunapokwenda mikoani kutoa uelewa na uwezesho wa masuala ya kisheria," alisema.

Alisema magari hayo yanatumia mafuta kidogo hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

RIPOTI MAALUM

# Taharuki wazazi na wanafunzi shule kufungwa zaidi ya mwaka

Na Mwandishi Wetu


SHULE inafungwa kwa mwaka mmoja na nusu, kupisha ujenzi. Zaidi ya wanafunzi 600, kuanzia darasa la awali hadi la saba wa shule hiyo, sasa hawana pa kusomea.

Hii ni Shule ya Awali na Msingi ya Rainbow iliyoko Toangoma, Kigamboni mkoani Dar es Salaam. Inamilikiwa na Kanisa la Tanzania Presbyterian (TPC) ikiwa na namba za usajili: PS 0206136 na ilianza kutoa huduma mwaka 2011.

Taarifa za kufungwa kwa shule hiyo zimethibitishwa na wazazi na walezi wa wanafunzi ambao Desemba 6, mwaka huu, walitumiwa ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) na uongozi wa shule. Ujumbe huo ulikuwa unawaarifu kwamba shule inafungwa kwa mwaka mmoja na nusu kuanzia Januari Mosi, 2025, hivyo watafute shule zingine kwa ajili ya watoto wao.

Mwandishi wa habari hii ameona ujumbe huo wenye maneno 155, kisha kumtafuta Meneja wa Shule, Mchungaji Hallington Kamanga, ambaye amekiri kuutuma kwa wazazi.

Ujumbe huo umetumwa kipindi ambacho shule zimekwishafungwa na usaili wa wanafunzi umeshafanyika kwenye shule nyingi. Licha ya kutangaza kuifunga shule hiyo, Mchungaji Kamanga hajaeleza hatima ya kimasomo kwa wanafunzi waliokuwa wakisoma shuleni hapo.




**USEMAVYO UJUMBE**

Ujumbe mfupi wa Mchungaji Kamanga uliotumwa kwa wazazi na walezi, ambao Nipashe imefanikiwa kuuona unasema: "Ndugu Mzazi/Mlezi, Shalom! Uongozi wa Kanisa la TPC umepokea Shule ya Rainbow mnamo 03/10/2024, ikiwa na idadi ndogo sana ya wanafunzi inayopelekea kukosa sifa ya kuwa kituo cha mtihani mwakani 2025.

"Kwa sababu hiyo, kanisa limekusudia kuanza na uboreshaji wa mazingira; kubomoa madarasa yaliyopoteza hadhi kwa kutofanyiwa maboresho kwa muda mrefu, na kujenga majengo mapya katika mfumo wa ghorofa.

"Tunapendekeza kusitisha masomo kwa madarasa ya elimu ya msingi kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu kupisha ujenzi na hivyo kukuomba wewe mzazi umtafutie mwanao shule nyingine.

"Ujenzi utakapokuwa umekamilika tutapokea wanafunzi tena na kuendelea na huduma ya elimu. Kwa kuwa wayajua vema mazingira ya shule jinsi yalivyo, tunatumai kuwa utaona umuhimu wa kile kinachokusudiwa kufanyika ili kuongeza hadhi, ubora na thamani ya shule kwa manufaa ya sasa na ya wakati ujao.

"Wanafunzi wa Chekechea (Pre-Primary) wataendelea na masomo. Wizara ya Elimu tayari imethibitisha jina jipya la shule na meneja tangu 19/11/2024. Sasa shule inaitwa "HEPHZIBAH PRE & PRIMARY SCHOOL."

Alipoulizwa sababu za kutoitisha kikao cha wazazi badala ya kutuma ujumbe huo, Mchungaji Kamanga anasema, hawezi kutoa ufafanuzi kwa kuwa jambo hilo limekuwa mahakamani kwa muda mrefu.

**TAHARUKI WAZAZI**

Kutokana na hali hiyo, sintofahamu imeibuka kwa wazazi na walezi ambao wamelalamikia uongozi wa shule kutoitisha kikao rasmi, jambo linalohusu hatima ya wanafunzi kielimu.

Baadhi ya wazazi wenye watoto shuleni hapo wameliambia gazeti hili kwamba baada ya kutumiwa ujumbe huo, waliomba kuonana na uongozi wa shule bila mafanikio.

Mama mwenye watoto wawili shuleni hapo, Magreth Kamaghe, anasema lengo la wazazi kuomba kuonana na uongozi ni kupata suluhu itakayowasaidia watoto wasiathirike kimasomo.

Anasema kabla ya ujumbe wa Mchungaji Kamanga, Septemba, mwaka huu walisikia tetesi za shule hiyo kufungwa lakini walipofuatilia kwa nyakati tofauti, uongozi wa shule na wa kanisa ulikanusha na kudai ni uzushi, huku wakiwataka waupuuze.

"Badala yake walituambia wanabadilisha menejimenti kwa kuleta nyingine mpya, lakini shule itaendelea kama kawaida. Kweli baada ya shule kufunguliwa ile Septemba, waliitisha kikao cha dharura na kuleta uongozi mpya, ambao ulituhakikishia kuwa shule haitafungwa," anasema.

Mzazi mwingine, Dk. Sixberth Mlowe, anasema wameshtushwa na uamuzi huo wa ghafla, licha ya kwamba wazazi na walezi walikuwa wanawasiliana na uongozi kila waliposikia tetesi.

"Ni uamuzi wa kikatili kwa watoto na wazazi. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba shule hii inamilikiwa na kanisa ambalo lina shule zingine za msingi, hawajataka kujali na kuwaza kuwahamishia watoto kwenye shule hizo nyingine, badala yake wameamua kuwafukuza," anasema.

Dk. Mlowe ameiomba serikali iingilie kati ili kunusuru hatima ya wanafunzi hao kielimu.

"Tunaona haya yanafanyika pengine kwa sababu wamiliki wa hii shule sio Watanzania, ni raia wa kigeni, lakini wanaoumia ni kizazi cha Tanzania.

"Kufukuza mtoto wa darasa la kwanza bila huruma ni kutojali taifa la kesho. Tunaiomba serikali iangalie kwa jicho la ziada ukatili huu, ili watoto hawa wasio na hatia, wapate haki yao ya elimu," anasema.

Alipoulizwa kuhusu uamuzi wa ghafla wa kuifunga shule, Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Dennis Mbiro, anasema yeye si msemaji wa suala hilo, bali uongozi wa kanisa kwa kuwa alikuwa anakaimu kwa kipindi cha mpito.

**MKURUGENZI WA SHULE**

Nipashe ilipomtafuta Mkurugenzi wa Shule za TPC, Pius Balihuta, kuzungumzia suala hilo, anasema uamuzi huo umefikiwa baada ya uongozi wa kanisa kushinda kesi iliyokuwa imefunguliwa na mchungaji aliyekuwa anasimamia shule hiyo.

"Mmishionari aliyepewa aisimamie alitaka aitoe kwenye umiliki wa kanisa ili iwe mali yake binafsi. Shauri likafunguliwa mahakamani ambako kanisa lilishinda kesi na kurudishiwa shule," anafafanua.

Anasema kesi hiyo ya madai namba 28/2022, ilifunguliwa na wachungaji Jung Hwan Kim na Sang Ok Nam, waliokuwa walalamikaji dhidi ya Bodi ya Wadhamini ya TPC waliokuwa washtakiwa.

Nakala ya hukumu ya kesi hiyo, ambayo Nipashe imeiona, ilitolewa Februari 5, mwaka huu, na Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Kigoma, John Nkwabi. Katika kesi hiyo, upande wa walalamikaji uliwakilishwa na Wakili Hamis Mbangwa na walalamikiwa uliwakilishwa na Wakili Paschal Kamala.

Hata hivyo, anasema licha ya mahakama kuirejesha shule kwenye uongozi wa kanisa mapema mwaka huu, uongozi wa kanisa haukuichukua shule hadi Septemba, mwaka huu.

"Kanisa limekuja na shauri moja la kuwaomba wazazi kama wataweza kuwahamisha watoto ili lifanye ujenzi mpya kwa maana ya kuvunja baadhi ya majengo na kujenga yanayofaa. Hatujawafukuza kwa sababu bado hatujafikia mwafaka," anasema.

Balihuta anasema hajaafiki ombi la wazazi la kuhamisha wanafunzi hao moja kwa moja kwenda shule nyingine ya TPC na badala yake, wameelekeza wafanye maombi ya kuhamia na kufanya usaili.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, utaratibu wa TPC ni kuchukua wale watakaofaulu mitihani ya usaili na si vinginevyo.

"Tumewaomba hao wazazi wawatafutie watoto shule zingine kwa mwaka mmoja na nusu, ili tufanye maboresho ya shule na baada ya hapo tutangaze kutafuta wanafunzi. Watakaofaulu ndio tutawachukua.

"Mzazi ambaye ataona ni sawa mtoto kusoma ujenzi ukiendelea, sisi tutamfundisha. Hatujawafukuza," anasema.

**SHULE NYINGINE**

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kwamba, miezi minane ya TPC kutoingiza menejimenti mpya shuleni Rainbow sasa Hephzibah, ulilenga kuwawezesha walalamikaji, Jung Hwan Kim na Sang Ok Nam, kujenga shule mpya.

Mmoja wa wazazi mwenye wanafunzi shuleni hapo, ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, anadai kilichotokea ni hujuma dhidi ya kizazi cha Tanzania.

Anasema TPC ilishirikiana na menejimenti ya zamani kuwezesha ujenzi wa shule mpya katika eneo la Kisarawe II, lililoko Kata ya Kisarawe, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, ambayo imesajiliwa kwa jina la Rainbow Junior Christian.

Anasema kutokana na jina la Rainbow kuhamia Kisarawe II, TPC imelazimika kuibadilisha shule ya Toangoma jina.

"Tunaona ni mkakati wa wazi wa hawa wamishionari kutoa huduma kwa mrengo wa kibiashara zaidi. Wamelindana na kuwezeshana, halafu wanaumiza watoto wa Tanzania," anasema.

Mzazi mwenye watoto wawili shuleni hapo ambaye naye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, anasema menejimenti iliyojenga shule mpya iliharibu shule ya awali kwa makusudi, huku uon-

*inaendelea uk. 7*

## Serikali yasisitiza kuboresha mazingira ufundishaji kidigitali

**Na Grace Mwakalinga**

SERIKALI imewahakikishia walimu kuwa itaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa kidijitali ili kuwawezesha kutimiza majukumu yao kwa weledi.

Mkakati huo ni sehemu ya hatua zinazochukuliwa kupitia Mradi wa Elimu ya Walimu (TESP), ulioanzishwa ili kuboresha ubora wa elimu ya walimu nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, katika mkutano na wadau wa elimu.

Prof. Nombo alisema mradi huo unalenga kuimarisha uwezo wa walimu na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya walimu nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo, kuanzishwa kwa vyumba vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na utoaji wa vifaa vya kisasa vya kidijitali.

"Utekelezaji wa mradi wa TESP umeleta maendeleo makubwa katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa kidijitali na hivyo kubadilisha mazingira ya vyuo vya walimu," alisema Prof. Nombo.

Alisema ujenzi wa chuo kipya cha Ualimu cha Kabanga, kilichojumuisha vipengele vya muundo wa kijani, ikiwa ni pamoja na kiwanda cha biogas kama chanzo cha nishati rafiki kwa mazingira, kimekuwa mfano mzuri wa muundo endelevu wa kijani.

Aliwashukuru wadau wa elimu, ikiwamo serikali ya Canada, kwa msaada wao katika utekelezaji wa mradi wa TESP ambapo alisema, umechangia kubadili mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji katika shule na vyuo vya walimu nchini.

"Mradi huu pia, unasaidia kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kukuza ujenzi wa majengo yanayozingatia ulinzi wa mazingira na kuhimiza matumizi ya nishati safi," alisisitiza.

Carol Mundle, Mkuu wa Ushirikiano wa Masuala ya Kimataifa wa Canada, alisema ni muhimu kuzingatia mabadiliko ya tabianchi katika elimu.

"Juhudi hizi zinakusudiwa si tu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi bali pia, kuhakikisha shule ni jumuishi na za haki," alisema Mundle.

Mratibu wa TESP, Cosmas Mahenge, alisema sekta ya elimu nchini imefanya mageuzi makubwa ya kimuundo yenye lengo la kuhakikisha elimu endelevu, jumuishi na yenye haki kwa wote.

Mradi wa TESP ulianza mwaka 2017 na unatarajiwa kumalizika mwaka 2025 ukiwa na bajeti ya Sh. bilioni 87.

# NSSF kujenga hoteli yenye hadhi ya nyota tano Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unatarajia kutumia takribani Sh. bilioni 148.4 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kitega uchumi jijini Dodoma, ambalo ni hoteli yenye hadhi ya nyota tano.

Mradi huo ambao utaanza rasmi kujengwa Mei, mwakani, faida ya uwekezaji huo italipa ndani ya miaka 11 na tayari mwendeshaji wa hoteli ameshapatikana.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa upandaji wa miti eneo la Njedengwa ambalo litajengwa vitega uchumi hivyo.

Alisema hatua hiyo ni utelekezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuwekeza majengo ya vitega uchumi katika jiji hilo na kwamba jengo hilo la hoteli litakuwa la ghorofa 16.

"Kwa sasa tunatafuta mkandarasi, hatua za awali zimeanza, tathmini za mwisho zitakamilika mwakani ili mradi uanze.

"Mwendesha hoteli ameshapatikana, hatutaki mradi huu hapa Dodoma tukosee, tumekuja kuwekeza hapa kwa sababu uwekezaji ni shughuli za msingi na tunaangalia maeneo ambayo tukiwekeza tunapata tunachotarajia ili tuendelee kulipa mafao," alisema.

> **"Ninamshukuru Rais kwa juhudi kubwa ambazo amekuwa akifanya katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini," alisema.**

Mshomba alisema mwaka jana, Rais Samia alipotembelea mradi wa Mwanza alivutiwa na uwekezaji huo akaagiza yaainishwe maeneo mengine nchini na baada ya kufanya tathmini kuwa italipa kwa vigezo vya uwekezaji.

Alisema mradi wa Mwanza unaendelea kwa kasi na mwakani utakamilika utavutia watalii Kanda ya Ziwa na mfuko utaendelea kukua.

"Ninamshukuru Rais kwa juhudi kubwa ambazo amekuwa akifanya katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini," alisema.

Alitaja mafanikio ya NSSF ndani ya miaka miwili chini ya uongozi wa Rais Samia kuwa ni pamoja na kuongezeka idadi ya wanachama, waajiri, ongezeko la michango hali inayochochea ukuaji wa mfuko na thamani ya mfuko imefikia zaidi ya Sh.trilioni 5.8.

"Moja ya kazi za NSSF ni kutunza fedha za wanachama ili kuhakikisha zimewekezwa kwa umakini mkubwa zitoe mapato ambayo yatawawezesha kutimiza malengo ya msingi ya kulipa mafao," alisema.

Pamoja na majukumu hayo ya msingi, Mshomba alisema uwekezaji huo ni jukumu la kipekee kwa sababu linatakiwa kufanyika kwa umakini mkubwa na kuzalisha kipato cha kutosha.

"Mafao ambayo NSSF tunalipa yanazidi michango ambayo mwanachama amechangia kwa kipindi chake cha utumishi, hivyo fedha hizo za ziada zitapatikana kupitia uwekezaji na ndio maana jambo hili ni muhimu sana.

"Kabla ya kujenga tulilazimika kupata vibali mbalimbali yote haya yamelenga kuhakikisha hatukosei, tunawekeza katika miradi ambayo inatupa faida," alisema.

Alisema wanawekeza katika miradi ambayo inaongeza mapato na kipaumbele cha usalama wa michango ya wanachama.

Kuhusu wajasiriamali walioko katika sekta isiyo rasmi, Mshomba alisema NSSF imejipanga kuweka mikakati itakayowawezesha kusajiliwa kwa wingi ili kuimarisha uchangiaji katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema uwekezaji huo wa NSSF mkoani humo utafungua fursa za mikutano mikubwa na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Awali, akitoa taarifa ya mradi, Meneja Usimamizi wa Miradi NSSF, Mhandisi Helmes Pantaleo, alisema jengo hilo litakuwa refu kuliko yote yaliyoko Dodoma.

Alisema wamefanya tathmini ya mazingira sambamba na kupima udongo ili kuangalia kama kuna hali ya tetemeko, mpango na ujenzi utachukua miaka mitatu na unatarajia kukamilika mwaka 2028.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Beatrice Banzi (kushoto), akimsikiliza mmoja wa washiriki katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji linalofanyika Saud Arabia juzi, baada ya kutembelea meza yao yenye bidhaa mbalimbali za chai inayozalishwa nchini, katikati ni Meneja Masoko wa Bodi hiyo, Selemani Chillo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulega akemea rushwa, ubabaishaji

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega, amekemea vitendo vya ubabaishaji na rushwa miongoni mwa watumishi wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kuwa vinaweza kufuta mazuri yote ambayo taasisi hiyo imeyafanya na inayoendelea kuyafanya.

Akizungumza na menejimenti ya TEMESA na mameneja wa mikoa jijini Dodoma jana, Waziri Ulega alisema serikali imedhamiria kuufanya wakala huo, kuwa taasisi namba moja na kimbilio la wote katika utengenezaji wa magari ya serikali na binafsi.

Ulega alisisitiza kuwa wanatakiwa kupiga vita vitendo vya ubabaishaji na rushwa na kubainisha kwamba huo ndio ugonjwa unaoharibu taasisi nyingi, hivyo wanatakiwa kutumia uwezo wao wote kupambana na jambo hilo.

"Pia hongereni kwa kuanzisha mkakati mpya wa kufanya kazi utakaowawezesha kujiendesha kibiashara kwa kushirikiana na sekta binafsi pale inapobidi ili kuihudumia jamii kikamilifu. Sisi TEMESA ni lazima tuwaoneshe watu ukinilipa nitakufanyia kazi kwa wakati," alisema Ulega.

Aliongeza kwa kuzisisitiza taasisi zingine za serikali zinazopatiwa huduma na wakala hiyo, kuweka mikakati ya kulipa madeni yao kwa wakati ili kuisaidia TEMESA kuondokana na madeni.

Aidha, alisema zaidi ya Sh. bilioni 67.4 zimetumika katika miaka mitatu ya serikali chini ya Samia Suluhu Hassan kujenga vivuko vipya sita, ukarabati wa vivuko saba na ujenzi wa miundombinu ya vivuko ambayo ni maegesho na majengo ya abiria katika Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi.

Ulega pia alipongeza ukarabati wa karakana za matengenezo ya magari unaoendelea kufanyika kote nchini na kusisitiza uendane na mabadiliko ya kimtazamo, utaalamu na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ili kuleta tija na ufanisi katika majukumu yao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kayoko kurudishwa kimya kimya ni kujenga matabaka kwa waamuzi

**DESEMBA12,** mwaka huu, kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, mashabiki walimshuhudia mwamuzi Ramadhani Kayoko, akirejea tena uwanjani kuchezesha mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya mwenyeji, Singida Black Stars na Dodoma Jiji FC.

Mwamuzi huyu alikuwa hajaonekana tangu achezeshe mchezo wa dabi, Simba na Yanga, Oktoba 19, mwaka huu, ambayo alivurunda kiasi cha Kamati ya Uendeshaji ya Bodi ya Ligi, ilipokutana pamoja na mambo mengine ilisema jambo lake, limepelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu ya Waamuzi baada ya kuonekana kutoutendea haki mchezo huo wa dabi.

Ilikuwa ni mwanzoni mwa mwezi Desemba ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi, Nassor Hamduni, alipothibitisha kuwa kuwa shauri la mwamuzi huyo limepelekwa kwenye kamati hiyo kwa ajili ya kujadiliwa na wajumbe wa kamati hiyo na kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya kufanyiwa maamuzi.

Hamduni aliahidi kuwa wangetoa kile ambacho kimeamriwa na wataalamu hao, lakini hadi leo hii hakuna kilichoendelea zaidi ya Kayoko kuonekana tena akichezesha.

Hadi leo mashabiki wameshindwa kujua kuwa ni kweli Kayoko alivurunda mchezo huo, au alichezesha kwa haki, ila ni mihemko tu ya mashabiki wa soka.

Wakati mashabiki wakisubiria jibu, kuonekana kwake tena akichezesha mchezo mwingine wa Ligi Kuu bila kuambiwa kuwa katika mchezo ule alifanya makosa au la, ni jambo ambalo tena lilikuwa likizua maswali mengi katika tasnia hii ya mpira wa miguu unaoongoza kwa kupendwa duniani.

Kila mpenzi wa soka alitegemea kabla ya Kayoko kuchezesha, kamati hiyo ingejitokeza na kutoa ushauri wake iliouita wa kitaalam kwamba ni kweli alifanya makosa na amefungiwa michezo kadhaa ambayo wangeitaja, na sasa imeisha anaruhusiwa kuchezesha.

Au hakufanya kosa lolote na kwa sababu wao ni wataalam walitazama dakika zote 90 na kujidhihirisha kuwa alikuwa sahihi, hivyo hawaoni sababu yoyote ya kuendelea kumsimamisha au kumfungia.

Kutolewa kwa moja kati ya maamuzi haya mawili wala kusingewashangaza wapenzi wa soka, badala yake wameonekana kushtushwa kumuona anachezesha tena bila kuambiwa kwanza lile kosa lake lililosababishwa apelekwe kwenye Kamati ya Waamuzi limeisha vipi.

Nipashe pia kama mdau mkubwa nchini wa soka, tunajiuliza ni kwa nini kumekuwa na ugumu wa kuliongelea suala la Kayoko kuliko mwamuzi mwingine yeyote.

Mbona huko nyuma waamuzi wamekuwa wakisimamishwa, wakifungiwa na baadaye kumaliza vifungo na kurejea uwanjani? Na wakati hayo yakiendelea mbona viongozi walikuwa wakijitokeza mbele ya kamera na vipaza sauti ya wanahabari kuelezea kufungiwa kwa marefa? Ni kwa nini kwa Kayoko limekuwa gumu?

Au kuna waamuzi maalum ambao wakipewa adhabu mambo yanakwenda kimya kimya na wengine wanatangazwa hadharani?

Hili kwetu tunaona ni kuweka matabaka. Sina uhakika mwamuzi atakayevurunda baadaye halafu atangazwe hadharani kuwa amefungiwa atajisikiaje wakati mwenzake Kayoko suala lake limeonekana kufichwafichwa, haijulikani kama alipata shauri la liliamuliwa vipi pasi vyombo vya habari kufahamishwa na kuuhabarisha umma.

Hili halijakaa sawa kuanzia kwa Kamati ya Uendeshaji ya Bodi ya Ligi na Kamati ya Nidhamu ya Waamuzi. Hata kama wamemrudisha lakini bado wana kitu cha kujibu hapa kuwa imekuwaje wakati wadau wa soka wanasubiri kujua kilichoamuliwa.

Au labda tuambiwe kuwa baada ya kelele nyingi za mashabiki kutuhumiwa kuvurunda mechi ya dabi, waliamua kumpumzisha kwanza ili ziishe na kumrudisha tena, na haya yote yaliyokuwa yakifanyika ni kutaka kuwapoza tu mashabiki.

Katika hili tunaona watakuwa wamepandikiza bomu kwa sababu ipo siku mwamuzi atafanya tena hivyo, halafu taratibu zikitaka kuchukuliwa wapo watakaowakumbusha kilichotokea kwa Kayoko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Soka la Wanawake linahitaji marekebisho, kuleta mvuto

**SI** siri kuwa Ligi Kuu Soka la Wanawake nchini imeanza kupendwa na mashabiki wengi nchini.

Hivi majuzi nilikuwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, maeneo ya Mwenge Dar es Salaam, ambapo kulikuwa na mchezo kati ya Yanga Princess na JKT Queens uliomalizika kwa Maafande hao kushinda mabao 2-0.

Ulikuwa ni mchezo mkali ambao haukuwa wa upande mmoja, badala yake timu zote zilipambana kuhakikisha zinapata ushindi.

Mchezo mwingine ambao niliushuhudia kabla ya huo uwanjani hapo hapo ni wa Simba Queens dhidi ya JKT Queens uliomalizisha kwa sare ya bao 1-1.

Maafande walipambana na kurudisha bao dakika za mwisho, ukamalizika kwa sare.

Nje ya uwanja, yaani majukwaani kulikuwa na mashabiki wengi ambao walikuwa wamechangamka, wakizishangilia timu hizo kwa ngoma, mavuvuzela na matarumbeta.

Haikutofautiana sana na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara za wanaume. Tena niseme tu hata baadhi ya mechi za Ligi Kuu Bara huwa hazina mvuto kama huo.

Mfano vile vikundi vya hamasa ambavyo huonekana kwenye timu kubwa za Simba na Yanga, huonekana pia kwenye mechi ambazo timu zao za wanawake zinacheza.

Hata mashabiki maarufu ambao wanaonekana wakati timu za wanaume zinacheza siku hizi huwakosi kwenye mechi za Ligi ya Wanawake.

Hii inaonesha kuwa soka la wanawake kwa sasa limeanza kuwa maarufu, na hata mitaani mashabiki wengi wa soka wanazifahamu pia timu za Ligi Kuu za wanawake na hata wachezaji wanaocheza ligi hiyo.

Ndiyo maana kuna wakati mchezaji fulani kama hayupo wanauliza yuko wapi? Ni kwa sababu tayari wanawafahamu.

Hata hivyo, pamoja na hayo kuna namna ambayo naona kama soka la wanawake halitendewi haki. Leo nimeangalia ratiba ndiyo angalau nimeona mechi zimefuatana angalau moja kwa wiki.

Kabla ya hapo, michezo ya wanawake ilikuwa ikichezwa wakati mwingine mara moja baada ya wiki mbili au tatu. Hii haileti afya hata kidogo kwa sababu hata mashabiki wanashindwa kuelewa.

Kwa watoto wa kike kucheza mechi moja baada ya wiki mbili au tatu hakuwafanyi wawe bora, badala yake wanakuwa wazito na kuonekana kama hawafanyi mazoezi, au viwango vimepungua.

Ushauri wangu ni kwamba mechi za Ligi ya Soka Wanawake ziwe zinachezwa kila wiki ili kuendelea kuwafanya mashabiki kula uhondo wa mechi hizo, lakini kuwaweka wachezaji katika hali ya ufiti.

Sidhani kama klabu huwa zinamudu kuwaweka kambini kama mechi zao zinachezwa wiki mbili au tatu mara moja. Badala yake zinawaruhusu kwenda kumpumzika majumbani na wakirejea wanakuwa kama wanaanza tena upya.

Inawezekana kabisa kuwa labda ni kwa sababu ya uchache wa timu zilizopo kwenye ligi hiyo.

Nashauri pia msimu ujao timu ziongezwe angalau ziwe 12 au 14 badala ya 10 ambazo zipo sasa.

Wachezaji wa kike hawana Kombe la FA, wana ligi tu, inakuwaje mchezaji acheze mechi 18 tu kwa msimu? Pamoja na kwamba baadhi wanakwenda kwenye vikosi vya timu za taifa, lakini idadi hii ya michezo haimpandishi kiwango mchezaji.

Pamoja na ugumu uliopo, lakini sasa ni wakati muafaka kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kusaka wadhamini kwa ajili ya soka la kinamama ambalo limeshaanza kukubalika.

Linaweza kuzitumia taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazoshughulika na haki za kinamama kusaidiana kushawishi kupata wadhamini kwa ajili ya kuboresha soka hilo ili liwe na mvuto zaidi na kuchezwa kama soka halisi la kulipwa.

# Taharuki wazazi na wanafunzi shule kufungwa zaidi ya mwaka

*Inatoka Uk. 4*

gozi wa TPC ukijua.

"Haiwezekani shule irudishwe TPC Februari, halafu waje waichukue rasmi Oktoba, miezi nane baadaye. Walikaa kimya makusudi wakimwezesha mchungaji wao aliyeshindwa kesi ili ajijenge. Waliacha hadi kufundisha watoto na kila tulipofuatilia, walisema wanashughulikia," anadai.

Anasema hali haikubadilika na kwamba, mwezi Julai, mwaka huu, walipata fununu kupitia kwa wanafunzi kuwa wamiliki wa shule hiyo, wanajenga shule nyingine.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Awali na Msingi Rainbow Junior Christian, Julieth Nzally, anafafanua madai hayo kwamba, ujenzi wa shule hiyo mpya una baraka zote za serikali na kwamba wamekubaliana na baadhi ya wazazi kuhamisha watoto.

SERIKALI YACHUNGUZA

Akizungumza na Nipashe kuhusiana na sintofahamu hiyo, Kamishna wa Elimu Tanzania, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema kilichofanyika shuleni hapo ni kinyume cha utaratibu, kanuni na mwongozo wa shule, unaotaka haki ya mtoto ilindwe katika mazingira yoyote.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mtahabwa amewaelekeza wadhibiti ubora kwenda kukagua shule hiyo ili kubaini chanzo cha kufungwa kwake.

Alisema uamuzi wowote haupaswi kuathiri wanafunzi na badala yake, uongozi huo unapaswa kuhakikisha maslahi ya wanafunzi kusoma yanalindwa.

**HUKUMU YA KESI**

Katika kesi hiyo, wachungaji hao Jung Hwan Kim na mkewe Sang Ok Nam, raia wa Korea Kusini, walishindwa kesi ambayo walikuwa wanadai fidia ya Sh. bilioni 1.4, walizodai walizitumia kujenga Shule ya Msingi ya Rainbow.

Hukumu hiyo iliyotolewa na Mahakama Kuu, Masjala Ndogo ya Dar es Salaam na walidai kuwa walijenga shule hiyo kwa fedha zao na michango kutoka kwa rafiki zao.

"Ninatamka kuwa mali Shule ya Rainbow na mali nyingine zote ni za Kanisa la Presbyterian Tanzania... nawaagiza Jung Hwan Kim na Sang Ok Nam kusalimisha usimamizi wa Shule ya Msingi ya Rainbow na mali zake zote kwa Kanisa la Presbyterian Tanzania," alisema Jaji John Nkwabi, katika hukumu yake ya Februari 5, mwaka huu.

Katika hukumu hiyo, Jaji Nkwabi alizingatia baadhi ya masuala, ikiwa ni pamoja na iwapo Wamishenari hao wawili walikuwa waanzilishi, wamiliki na wafadhili wa shule ya Rainbow. Alizingatia kama Rainbow ulikuwa mradi wao chini ya mwavuli wa TPC.

Jaji Nkwabi alisema cheti cha usajili wa shule hiyo kinaonesha kuwa mmiliki ni TPC, huku msimamizi wa shule hiyo akiwa ni Jung Hwan Kim.

Pia alisema Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) pamoja na hati ya eneo shule ilipojengwa vipo kwa jina la Tanzania Presbyterian Church.

"Hiyo inathibitisha vya kutosha kuwa mshtakiwa (Kanisa la Presbyterian Tanzania) ndiye mmiliki wa shule. Walalamikaji (Jung Hwan Kim na Sang Ok Nam), wameshindwa kuthibitisha kuwa wanamiliki shule hiyo," aliamua.

"Kwa vyovyote vile, alisema, ushahidi wa mashahidi wa walalamikaji unaonekana kuwa na chuki dhidi ya mshtakiwa kwa sababu walifukuzwa kazi katika Shule ya Awali na Msingi ya Philadelphia ambayo pia, iko chini ya mshtakiwa (TPC)."

Aidha, alisema ni jambo lisilowezekana ingawa walalamikaji wanaeleza kuwa stakabadhi hizo hazipo katika majina yao bali zipo kwenye jina la shule, wanataka kulipwa fidia na mshtakiwa ya Sh. 1,417,152,600 bila uthibitisho wowote kama walitumia fedha zao.

Alisema sheria hairuhusu fidia hiyo kulipwa kwa kuwa inataka upande wa mlalamikaji kuthibitisha tuhuma ilizowasilishwa mahakamani.



Watumishi kutoka Dawati la Msaada wa Kisheria Dar es Salaam (kushoto), wakiwasikiliza baadhi ya wakazi wa mtaa wa Amani, Kata ya Kipunguni, walipofika eneo hilo jana, kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mhudumu wa baa aachiwa huru kesi dawa za kulevya

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imemwachia huru mhudumu wa baa, Ashura Kaoga, baada ya kumwona hana hatia na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha shtaka la kusafirisha dawa za kulevya dhidi yake.

Mhudumu huyo aliachiwa huru mbele ya Jaji Sedikia Kisanya baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na kujiridhisha kwamba Jamhuri ilishindwa kuthibitisha shtaka la kusafirisha kilo 321.10 za bangi lililokuwa likimkabili.

Ilidaiwa Oktoba 10,2023 katika Kijiji cha Nkerege wilayani Tarime, Mkoa wa Mara mshtakiwa alikutwa na kilo 321.10 za bangi.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Angela Chacha, Mafuru Moses na Wakili wa Serikali Davis Katesigwa na waliita mashahidi watano na vielelezo vinane.

Upande wa utetezi uliita mashahidi watatu na mshtakiwa aliwakilishwa na Wakili Juma Mwita.

Upande wa mashtaka katika Ushahidi, ulidai kuwa Oktoba 2, 2023 saa 4:00 asubuhi, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Kanyumbu akiwa na askari wengine wakiwa Kijiji cha Nkerege walipata taarifa ya mtuhumiwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Ilidaiwa walifahamishwa mtuhumiwa amelala nyumba ya wageni inayoitwa Kwa Matete na askari walifika wakakamilisha taratibu zikiwamo kujitambulisha na kufanya upekuzi katika chumba alichokuwamo mshtakiwa lakini hawakukuta kitu.

Upande wa mashtaka ulidai mshtakiwa alimpeleka askari porini kilomita nne kutoka walipokuwa na walipofanya upekuzi huko, walikuta viroba 14 vyenye majani makavu yaliyodhaniwa kuwa ni bangi na yalipofanyiwa uchunguzi, ilibainika kuwa ni bangi.

Katika utetezi, mshtakiwa alikubali kwamba alikamatwa akiwa nyumba ya kulala wageni ya Kwa Matete na ushahidi wake uliungwa mkono na ushahidi wa shahidi wa pili, wa tatu na wa nne wa upande wa utetezi.

Ushahidi wa upande wa utetezi ulidai kwamba mshtakiwa ni mhudumu wa baa kwa Burule jirani na nyumba ya kulala wageni ya Kwa Matete.

Mshtakiwa alidai katika nyumba hiyo ya kulala wageni alikwenda kukutana na shahidi wa tatu wa upande wa utetezi ambaye walikubaliana kwenda kwenye starehe usiku huo.

Mashahidi wote wa upande wa utetezi walidai asubuhi askari waligonga mlango na kujitambulisha, walifanya upekuzi na hawakukuta kitu chochote pia waliwatoa nje kuelekea kwenye gari kisha kuondoka nao.

Ilidaiwa walipowafikisha walipotaka wao waliwaonyesha viroba vingi, walipewa fungu la viroba ambavyo hawakuvitambua.

Jaji Kisanya alisema Mahakama imezingatia ushahidi wa pande zote mbili hakuna ubishi kwamba bangi ilikutwa porini na si katika eneo alilokamatwa mshtakiwa.

"Upande wa Jamhuri umeegemea katika ushahidi wa shahidi wa pili na maelezo ya onyo ikidaiwa mshtakiwa aliwapeleka polisi porini lakini mshtakiwa alikana. Alidai viroba walivikuta mahali ambapo askari waliwapeleka na kwamba vilifikishwa hapo kwa gari.

"Mshtakiwa alidai ni mhudumu wa baa ya Burule na alikamatwa akiwa chumbani katika nyumba ya kulala wageni ya Kwa Matete. "Kwa kutenda haki katika shtaka la kusafirisha dawa za kulevya linalomkabili mtuhumiwa, ni muhimu kutathmini kama mshtakiwa alikodi chumba kwenye nyumba ya wageni ya Kwa Matete.

"Muhimu kutathmini kama alikiri kujihusisha na dawa za kulevya, na kuwaongoza maofisa hadi porini ambako shahidi wa pili upande wa mashtaka alimkuta akiwa na viroba 14 vyenye majani yaliyodaiwa ni bangi.

"Tukianza na hoja iwapo mshtakiwa alikuwa amekodisha chumba, alikodi kwa nia ya kujihusisha na dawa za kulevya kuna walakini.

"Mbali na ushahidi wa shahidi wa pili wa upande wa mashtaka kwamba mshtakiwa alikuwa mteja na si mhudumu wa baa ya jirani ambaye alienda huko kukutana na shahidi wa tatu wa upande wa utetezi kama mashahidi wa upande wa utetezi walivyodai, hakuna mtu mwingine anayeunga mkono ushahidi wa shahidi wa pili," alisema Jaji.

Alisema upande wa mashtaka haukumleta Jesca Magesa, ofisa huyo ambaye shahidi wa pili alidai alisaidia katika kukamata na kupekua. Kama vile hiyo haikutosha, mhudumu wa nyumba ya wageni, ambaye aliwaongoza hadi chumba ambacho kilidaiwa kukodishwa na mshtakiwa hakuitwa kama shahidi.

" Upande wa mashtaka ulitakiwa kuleta ushahidi wa ziada kuhusu mtuhumiwa, wangeweza kuchunguza maelezo kama vile alikotoka, siku aliyofika kwenye nyumba ya wageni, alifika na nini, alileta nini na alilipa kiasi gani chumba. Ushahidi huu ungeweza kufafanua kama mshtakiwa kweli alikodisha chumba katika nyumba ya wageni ya Kwa Matete na si mhudumu wa baa kwenye baa iliyo karibu ya Burure," alisema Jaji Kisanya.

Alisema hakuna idadi maalum ya mashahidi inayohitajika kuthibitisha kesi

na kwamba kupuuza kuita mashahidi muhimu bila maelezo ya kuridhisha, yanadhoofisha kesi ya mhusika.

"Katika shauri hili upande wa mashtaka sio tu ulishindwa kuita mhudumu wa nyumba ya wageni ambaye aliwaongoza kwenye chumba lakini pia ulipuuza kumleta Damary Daniel Magige, shahidi aliyeorodheshwa kutoka katika nyumba hiyo ya wageni.

"Hapana sababu ya msingi iliyotolewa kwa kushindwa huku, matokeo yake Damary aliitwa kutoa ushahidi kwa upande wa utetezi, ushahidi wake ulionyesha kuwa mshtakiwa alikuwa mhudumu wa baa katika baa ya karibu ijulikanayo Kwa Burule na kwamba alipatikana tu katika nyumba ya kulala wageni ya Kwa Matete alipoenda kulala na Thomas shahidi wa tatu upande wa utetezi.

"Katika hali hiyo, sioni sababu ya kudhoofisha ushahidi wake, nahitimisha kuwa upande wa mashtaka ulishindwa kuthibitisha kwamba mtuhumiwa alikuwa amekodisha chumba katika nyumba ya wageni inayohusika.

"Upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha shtaka bila kuacha shaka dhidi ya mshtakiwa, ushahidi hauridhishi, Mahakama inamuona mshtakiwa hana hatia na inamwachia huru," alisema Jaji Kisanya.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# DC aagiza vishoka kutimuliwa Sirari

**Na Samson Chacha** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Meja Edward Gowele, amewaagiza maofisa wa serikali walioko katika kituo cha forodha cha Sirari kuwaondoa mara moja mawakala bandia, maarufu kama 'vishoka' ili kudhibiti upotevu wa mapato.

Meja Gowele alitoa agizo hilo juzi kwa maofisa hao wa serikali kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Uhamiaji, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Vipimo (WMA), Mawakala wa Uondoaji Mizigo sekta za afya, kilimo na uvuvi.

Alisema ili kuwezesha upatikanaji mapato katika eneo hilo la mpaka ni lazima watumishi wa umma watekeleze majukumu yao ipasavyo kwa kuwa kila kitengo kimewekwa katika eneo hilo na hakuna haja ya kuwapo kwa vishoka hao.

"Waondoeni madalali hawa wanaofanya shughuli katika forodha bila kuwa na sifa. Hawana vitambulisho wala ofisi zinazotambuliwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC).

"Mawakala mlio katika kampuni zilizosajiliwa kihalali mnatakiwa kuwa waadilifu katika kutoa huduma katika maeneo ya umma kwa kushirikiana na watumishi wa idara mbalimbali waliopo hapa ili kufanikisha utendaji kazi kati ya kampuni zenu na serikali kwa kufata taratibu na sheria za nchi ili kuepuka ujanja ujanja ambao unakosesha serikali mapato," alisema.

Meja Gowele alisema kuendelea kuwapo kwa vishoka hao, kunachangia migogoro ya mara kwa mara pamoja na upotevu wa mapato serikalini.

Awali, Mtakwimu Mwandamizi wa TASAC, Athuman Athuman, alikiri kuwapo kwa vishoka wanaofanyakazi ya uwakala bila kusajiliwa , hivyo wanavunja sheria za nchi.

"Tutafuatilia pia kampuni zote zinazoshirikiana na watu hao wasio na sifa za uwakala bila kufata utaratibu ili hatua kali zichukuliwe kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali na kuingia mifukoni mwa kikundi cha wanaohujumu uchumi wa taifa," alisema Athuman.

Kaimu Meneja wa Kituo cha Forodha Sirari, Abdallah Salum, aliwataka mawakala walioko katika eneo hilo kutoa ushirikiano kwa watumishi wa umma ili kufanikisha utendaji kazi kati yao na mawakala.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya uwakala wa forodha, Maryan Muhambo, aliiomba TASAC kuwa na utaratibu wa kuwatembelea na kutoa elimu kwa kampuni za mawakala forodhani na kukusanya kero zinazowakabili ili kufanikisha utendaji kazi.

# Bwawa la umeme JNHPP lakamilika asilimia 99.5

**Na Joseph Mwendapole**

UJENZI wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP) lililoko Rufiji mkoani Pwani, umefikia asilimia 99.5 ya utekelezaji wake na wakati wowote mitambo yote itawashwa na kuingizwa umeme kwenye gridi ya taifa.

Bwawa hilo litakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 mitambo yake yote tisa itakapowashwa na kuanza uzalishaji, hivyo kuondoa kero ya umeme.

Jana uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ulitembelea mradi huo kujionea kasi ya maendeleo ya ujenzi na kuweka mkazo kwa wasimamizi kuhakikisha usimikaji wa mashine nne zilizobaki unafanyika haraka.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Boniface Nyamo-Hanga, alisema kwa sasa mashine tano zimekamilika kwa asilimia 100 ambazo ni mashine namba 9, 8, 7, 6 na 5 na tayari zimeanza uzalishaji wa umeme.

"Tumetembelea mradi huu kujionea shughuli zinazoendelea na kuweka msisitizo wa usimamizi bora kwa maeneo ambayo bado hayajakamilika. Utekelezaji kwa ujumla umefikia asilimia 99.5 huku shughuli za uzalishaji wa umeme zikiwa zimeanza na wastani wa megawati 1,175 zinazozalishwa kutoka mashine tano zimeingizwa kwenye gridi ya taifa," alisema.

Alibainisha kuwa utekelezaji wa usimikaji wa mashine namba nne umefikia asilimia 100 na sasa mashine iko kwenye majaribio huku mashine namba tatu ikiwa kwenye asilimia 87 za usimikwaji.

**"Niwaombe msimamie vizuri kuhakikisha ufanyaji kazi wa mashine unakuwa mzuri ili umeme unaoendelea kuzalishwa unapoungwa kwenye Gridi ya Taifa usilete changamoto..."**

Nyamo-Hanga aliwahimiza wasimamizi wa mradi kuhakikisha wanaongeza bidii kusimamia maeneo ambayo bado hayajakamilika na kazi inafanyika kwa viwango vilivyoainishwa wakati wa usanifu wa mradi.

"Niwaombe msimamie vizuri kuhakikisha ufanyaji kazi wa mashine unakuwa mzuri ili umeme unaoendelea kuzalishwa unapoungwa kwenye Gridi ya Taifa usilete changamoto yoyote," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Nyamo-Hanga aliishukuru serikali ya awamu ya sita, Wizara ya Nishati na viongozi wake wote kwa namna ambavyo mara zote wamelipa shirika fedha.

Alisema serikali imeonyesha ushirikiano mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa mradi huo mpaka kufikia hatua iliyopo sasa pamoja na miradi mingine mingi inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali nchini .

"Ninawaahidi Watanzania wenzangu kuwa sisi viongozi wa TANESCO tutahakikisha tunasimamia mradi huu kwa dhati na umadhubuti mkubwa ili ukamilike kwa wakati na kuleta tija ya kiuchumi na kijamii katika taifa," alisema.

Mradi wa bwawa la kufua umeme wa JNHPP tayari umeanza kuleta matumaini makubwa ya kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini ikiwa ni kati ya juhudi kubwa zilizofanywa na serikali ya awamu ya sita.



Baadhi ya wahandisi wazawa wakiwa katika mkutano wa kukusanya maoni ya mabadiliko ya sheria ya uhandisi yaliofanyika jijini Dar es Salaam, ulioandaliwa na Wizara ya Ujenzi na Bodi ya Wahandisi Tanzania (ERB) jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TBA yataka sekta ya fedha iwe nguzo kuu ya dira 2050

**Na Maulid Mmbaga**

UMOJA wa Benki Tanzania (TBA) umependekeza sekta ya fedha kuwa miongoni mwa nguzo kuu katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kutokana na umuhimu wake katika kuchochea ukuaji wa uchumi nchini, ikieleza kuwa kuna takriban malengo 16 ambayo fedha inaweza kuchangia katika ufanikishaji wa dira.

Akizungumza juzi mkoani Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa taasisi za fedha kuhusu kuhakiki rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mkurugenzi Mtendaji wa TBA, Tusekelege Joune, alisema wanatamani kuona sekta hiyo inakuwa moja ya nguzi kwasababu wameona mifano mingi katika mataifa yaliyoendelea.

Alisema wangetamani pia kuona mambo mawili yakifanyika ikiwamo usaidizi usioyumba wa serikali kwenye sekta hiyo katika masuala ya sera, sheria na hatua za kiutawala kwa kuwa itasaidia taifa kupiga hatua ya kimaendeleo.

"Kwa nini tunatamani kuona sekta ya fedha kuwa moja ya nguzo? Ni kwa sababu tukichukulia hali ya ukuaji wa uchumi wa Uingereza katika karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20, ilikuwa wakati huo ambako benki na taasisi za fedha zilianua ukuaji na mwelekeo wa rasilimali za kifedha.

"Hiyo ilisaidia serikali kusaidia uzalishaji, usambazaji, mifumo ya kubadilishana biashara za kimataifa na ubia.

Tumeona kuongezeka kwa China, Singapore, Brazil, na Malaysia. Tunapoyaangalia haya yote, tunaona kwamba yamejikita katika kupima sekta ya fedha katika mwelekeo wa usaidizi. Wametoa kipaumbele maalum kwa sekta ya benki," alisema.

Aliongeza kuwa sekta ya fedha ndiyo chachu, kichocheo, na kiwezeshi cha ukuaji wa uchumi.

Kwa hivyo hiyo ilikuwa moja ya matakwa yao makubwa kuona yakipewa kipaumbele katika maono ya dira 2050.

Pia alisema muundo wa dira una nguzo za kimsingi, ambazo zote ni muhimu kwa maendeleo ya baadaye ya sekta ya fedha. Ambako ukuaji wa uchumi, rasilimali watu na mabadiliko ya hali ya hewa ni sehemu yake. Akieleza kuwa baada ya muda kutahitajika jukumu la ufadhili katika kufikia matokeo ya muda mrefu.

Hata hivyo, alisema utaratibu huo utasababisha sekta ya fedha kuunganishwa na sekta za kipaumbele na kutoa thamani bora kwa kipindi chote cha mradi mpya, katika kufikia malengo ya maendeleo na uchumi imara, shirikishi na wenye ushindani.

"Uchumi unaostawi mara nyingi hufaidika na sekta ya fedha iliyochangamka.

Tamaa hii inasukuma sekta hii kufikiria upya jukumu lake katika dhana ya mabadiliko, kwa matarajio ya ajenda ya kiuchumi. Inatia moyo sana kujifunza kuhusu umuhimu mkubwa wa maendeleo na masuala ya hali ya hewa ndani ya dira ya 2050.

"Hili si tu muhimu kwa sekta nzima ya fedha, lakini pia ni muhimu sana kwa uendelevu wa siku zijazo na matokeo ya muda mrefu ya Dira ya 2050 ambayo inalenga kuafikiwa. Kama sekta nyingine yoyote, pia sekta hii inahitaji wafanyakazi wenye uwezo ili kuhudumia mahitaji ya uchumi, biashara na kaya," alisema.



# TUGHE yaja na hoja sita kwa serikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) kimetoa hoja sita kwa serikali ikiwamo kuomba ufanyike ukaguzi kwa sekta binafsi ili kukomesha unyanyasaji wafanyakazi na kupata ajira za kudumu.

Hoja hizo zimo kwenye risala ya TUGHE iliyosomwa jana kwenye Mkutano Mkuu wa chama hicho sambamba na Maadhimisho ya Miaka 30 tangu kuanzishwa.

Akisoma risala hiyo, Katibu Mkuu TUGHE, Hery Mkunda, alisema ukaguzi huo utasaidia kubaini ukubwa wa tatizo na kufanya marejeo ya sheria ili kuboresha mikataba ya ajira na adhabu kwa waajiri wanaozuia wafanyakazi kujiunga na vyama vyao.

"TUGHE tunawakilisha wafanyakazi toka katika taasisi binafsi zinazotoa huduma ya afya. Katika taasisi hizi pamoja na nyingine binafsi, imekuwapo changamoto kubwa ya muda mrefu ya wafanyakazi kukosa ulinzi wa ajira zao,"alisema.

> **"Waajiri wengi katika sekta binafsi hutumia aina hii ya ajira za mikataba ya muda mfupi kuwanyima wafanyakazi wao baadhi ya haki na stahili kama vile kutowachangia katika mifuko ...**

Alisema ajira nyingi katika sekta binafsi ni za mikataba ya muda mfupi kuanzia za vibarua. Alisema ajira hizo kuanzia mwezi mmoja hadi miezi mitatu, zinawanyima uhakika wa ajira zao.

"Waajiri wengi katika sekta binafsi hutumia aina hii ya ajira za mikataba ya muda mfupi kuwanyima wafanyakazi wao baadhi ya haki na stahili kama vile kutowachangia katika mifuko ya hifadhi ya jamii, bima za afya, kutowapatia likizo ya mwaka, uzazi, kuugua, dharura kwa mujibu wa sheria na kutowalipa mshahara kwa saa za ziada na saa za kazi za usiku," alisema.

Alisema ili kukwepa mkono wa sheria hasa maofisa wa kazi wanapofanya kaguzi, waajiri wenye tabia hizo wamekuwa wakiwabadilishia majina wafanyakazi katika kila mkataba ili waonekane kuwa ni wapya.

"Changamoto nyingine ni uwapo wa wabia ya baadhi ya waajiri serikalini kuwahamisha viongozi wa matawi ya vyama vya wafanyakazi mahala pa kazi kwa lengo la kuwadhoofisha wanapoonekana kuwa na ushawishi mkubwa katika utetezi wa watumishi wengine,"alisema.

Alisema changamoto nyingine ni uwapo wa baadhi ya taasisi za umma ambazo waajiri wanaitikia wito wa kuunda mabaraza ya wafanyakazi, lakini uendeshaji wa vikao hauzingatii sheria na kanuni.

Akifungua mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Zuhura Yunus, alisema serikali imepokea na itafanyia kazi hoja hizo. "Mmependekeza wizara iongeze bajeti na idadi ya wafanyakazi katika idara ya ukaguzi kwa lengo la kuboresha kaguzi maeneo ya kazi. Hili nimelipokea na litazingatiwa wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26," alisema Zuhura.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji (wa pili kushoto), akilisha samaki chakula juzi, kwenye moja ya vizimba vilivyotolewa na serikali kwa mkopo wenye masharti nafuu eneo la Lake Side, mkoani Mara. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evansi Mtambi na Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, Vedastus Matayo (kulia kwake). Wengine ni Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji, Dk. Nazael Madala (kulia) na Mmoja wa wanufaika wa vizimba hivyo, Godwin Kibabaye. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE.**

# Wazazi wahimizwa kulinda watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

KAMATI ya Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wilayani hapa Mkoa wa Singida imewataka wazazi na walezi kuwalinda watoto katika kipindi hiki cha likizo dhidi ya vitendo vya ukatili.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa MTAKUWWA, Robby Muhochi, alitoa wito huo juzi wakati wa kikao cha kujadili taarifa za utekelezaji wa miradi kutoka divisheni ya maendeleo ya jamii katika huduma ya afya, ustawi wa jamii na lishe. Akitoa taarifa ya mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, Muhochi, alisema wakati wa likizo kuna mkusanyiko wa watu majumbani na mtaani, hivyo wanapokwenda kucheza walindwe wasifanyiwe vitendo hivyo.

Alisema kumekuwa na tatizo kwa jamii kutokutoa ushirikiano kuhusiana na waathirika wa ukatili na kutoshiriki katika mikutano inayotoa elimu dhidi ya vitendo hivyo.

Wakitoa maoni yao katika kikao hicho, wajumbe walipendekeza elimu iendelee kutolewa kwa jamii ilikuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na huduma ya mkono kwa mkono kuchukua mkondo wake.

Mikakati mingine iliyowekwa ni kuendelea kudhibiti matukio hayo wilayani hapa kwa kamati za MTAKUWWA kukutana na kujadili namna ya kutokomeza janga hilo.

Kuhamasisha wananchi kutoa taarifa za ukatili, kuhamasisha wananchi kushiriki mikutano ya elimu dhidi ya matukio hayo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Haika Massawe, alisema kuna haja ya wazazi kupewa elimu hasa kipindi hiki cha likizo watoto wanapokua nyumbani kwani ndiko yanakotokea matukio ya ukatili.

# Jamii yaombwa kuwakumbuka wahitaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JAMII imeombwa kuwakumbuka watu wenye mahitaji wakati huu wa kuelekea sikukuu ya krismasi na mwaka mpya kwa kuwapatia misaada ili wafurahie kama ilivyo kwa watu wengine.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wazee wanaotunzwa na Kituo cha Mather Tereza cha Hombolo Bwawani jijini hapa baada ya kupokea msaada kutoka Kampuni ya Jumaco Property Limited.

Akizungumza baada ya kupokea zawadi hizo kwa niaba ya wazee wenzake, Mathonya Yohana (75), aliwaomba wananchi kuwakumbuka watu wenye uhitaji kwenye kipindi hiki cha sikukuu hizo ili na wao wajione sehemu ya jamii yenye kufurahia.

Alisema watu wenye uhitaji wamekuwa wakisahaulika katika jamii, hivyo mashirika, taasisi na watu binafsi wanapaswa kuwakumbuka na kuwasaidia.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Julius Harweri, alisema jamii inawajibu kuwakumbuka watu wenye uhitaji mara kwa mara na kupunguza changamoto wanazokabilianazo.

Kampuni hiyo mbali ya kuwapatia msaada huo kwa watu wenye uhitaji wakiwamo watoto na wazee wanaotunzwa kwenye kituo hicho pia walishiriki chakula cha pamoja.

# TAKUKURU yatangaza vipaumbele

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapa imetaja vipaumbele saba vya utekelezaji majukumu yake ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha zinazotolewa na serikali kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Victor Swella alivitaja vipaumbele hivyo taarifa yake ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi kijacho.

Kwa mujibu wa Swella, vipaumbele hivyo ni kuongeza kasi ya uelimishaji madhara ya rushwa katika makundi tofauti ili kuwawezesha wananchi kujua wajibu wao wa kuzuia.

Kuongeza kasi ya uelimishaji kwa kutumia njia mbalimbali hususani katika makundi ya vijana ambao ndio nguvu ya taifa na viongozi wa baadaye.

Kuongeza kasi ya kufanya chambuzi za mifumo maeneo yanayolalamikiwa zaidi kwenye utoaji huduma kwa wananchi.

Kuendelea kuelimisha jamii hususani kundi la vijana kupitia ushirikiano uliopo kati ya taasisi hiyo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya mkoani hapa.

Kuongeza kasi ya kuwafikia wadau kupitia programu ya TAKUKURU rafiki ili kuibua kero zao na kuzipatia ufumbuzi.



# TIA yajenga kampasi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa kiasi cha Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya Uhasibu nchini (TIA) Kampasi ya Zanzibar ili kutoa fursa zaidi ya wanafunzi kujiunga ndani na nje ya nchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa Willian Amos Pallangyo, aliyasema hayo baada ya kukagua awamu ya kwanza ya ujenzi huo unaendelea eneo la Makunduchi Ng'anani Mkoa wa Kusini Unguja.

Pallangyo, alisema ujenzi huo ulianza Septemba mwaka huu baada ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kutoa fedha hizo na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) eneo lenye ukubwa wa hekari 56.

Alisema watahakikisha fedha hizo zilizotolewa na serikali zinatumika vizuri na kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Alisema ujenzi huo unaambatana na wa kumbi za mihadhara, vyumba vya maktaba, kompyuta na mabweni ya wanafunzi wa kike na kiume.

Naibu Mkuu wa Mipango, Fedha na Utawala, Dk. Issaya Hassanal, alisema ujenzi wa kampasi hiyo utakamilika mwaka 2026 na kuanza kupokea wanafunzi wa ndani na nje ya nchi kupata elimu na kutoa wataalamu waliobobea katika fani za uhasibu, ukaguzi wa hesabu na nyingine zinatolewa na taasisi hiyo.

Hassanal, alisema ujenzi huo utasaidia kutoa ajira kwa wananchi wanaoishi maeneo jirani, wakiwamo mamalishe na babalishe na kujiongezea kipato katika familia zao.

Mhandisi wa ujenzi wa mradi huo, kutoka Kampuni ya Salem Constructions, Riziki Ringo, alisema wanatarajia kukamilisha katika kipindi cha miaka miwili kwa mujibu wa mkataba na taasisi hiyo, licha ya kuwapo kwa changamoto ndogo ndogo.

# Rais Mwinyi awajibu wanaombeza

## -Azindua ujenzi barabara ya juu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ujenzi wa barabara ya juu ni alama ya kudumu kwa visiwani hapa tangu mapinduzi na kuwapasha wanaombeza kwa sasa wataona maendeleo ya angani baada ya kukamilisha ya ardhini.

Mwinyi alitoa kauli hiyo wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara hiyo kwanza kwa Zanzibar katika eneo la Mwanakwerekwe.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, aliwajibu wanaompa majina ya kumbeza kutokana na maendeleo anayafanya Zanzibar.

Mwinyi, alisema watu hao sasa watapata jina jipya kutokana na ujenzi wa barabara hiyo ya juu.

Alisema wale ambao hawaoni maendeleo yaliyopo ardhini sasa waangalie angani na kama yote hayo hawayaoni huo utakuwa ni ujuha.

Alisema maendeleo kwa kazi ya angani sasa imeanza na mambo mazuri zaidi yanakuja kwa Zanzibar.

> **"Yale tuliyoyaahidi tumevuka na sasa tunaendelea kutekeleza yale ambayo hayamo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020/2025,"**

Mwinyi alirejea msemo wake kuwa yajayo ni neema zaidi kuwa ana mipango madhubuti ya kupanda fedha ili kuleta maendeleo kila upande.

"Pale tunaposema tuwe na uongozi wa kuacha alama na kusudia haya, hii ni alama ya kudumu kwa kweli tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuyafanya haya tuliyowaahidi wananchi," alisema Mwinyi.

Aliisifu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara na madaraja katika visiwa vya Pemba na Unguja na kuharakisha maendeleo kwa wananchi.

"Yale tuliyoyaahidi tumevuka na sasa tunaendelea kutekeleza yale ambayo hayamo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020/2025," alisema na kusisitiza kuwa mambo mazuri zaidi yanakuja.

Mwinyi, alisema serikali yake ina mipango madhubuti na thabiti ya kupata fedha kwa ajili ya kuendelea kuijenga Zanzibar na kuwa na maendeleo.

Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Khalid Muhamed, alisema serikali inajenga kilomita 897.2 za barabara katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Muhamed, alisema barabara hizo zinajengwa katika umbali wa kilomita 1,344, kazi kubwa ambao haijawahi kutokea tangu wakati wa mapinduzi hayo.

Alisema pia serikali inatarajia kujenga madaraja kuunganisha Kijiji cha Chwaka na Charawe pamoja na Uzi na Unguja Ukuu vinavyozungukwa na bahari.

Vilevile, alisema serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya kilomita 15 katika kisiwa cha Tumbatu.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Makame Haji Machano, alisema ujenzi wa barabara hiyo ya juu ni sehemu ya mradi wa barabara za mjini za kilomita 100.9.

Machano, alisema ujenzi huo unajumuisha barabara za juu mbili za Mwanakwerekwe na Amani kwa kisiwa cha Unguja.

Alisema ujenzi huo una lengo la kudhibiti msongamano barabarani kutokana na ongezeko la vyombo vya moto na kurahisisha shughuli za uchumi.

Alisema ujenzi huo kwa awamu ya kwanza, ulianza rasmi Desemba 1, mwaka 2022 na unatarajiwa kukamilika Machi 20, mwakani.

Alisema Sh. bilioni 2.7 zilitumika kuwalipa wananchi fidia waliopisha maeneo yao na kuruhusu kuanza kwa ujenzi huo ambao umefikia asilimia 80.



Wakazi wa Kivule jijini Dar es Salaam wakichuma mboga katika bustani yao jana, kwa ajili ya kutembeza mitaani kusaka wateja kwa bei ya Sh. 200 kila fungu ambalo sokoni huuzwa kwa Sh. 500. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mgongano wa maslahi waikosesha serikali mapato miezi saba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MVUTANO wa maslahi umeibuka baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Manispaa ya Mjini na kusababisha Kampuni ya Simba Developer kushindwa kuwasilisha asilimia 25 serikalini ya makusanyo ya mapato kwa miezi saba.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Mipango na Bajeti wa Baraza la Manispaa Mji wa Zanzibar, Rahma Ali Khamis, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa robo ya kwanza katika kikao cha baraza la mji huo.

Rahma, alisema wizara hiyo inadai kuwa ni wamiliki wa eneo la shule na kutaka wajumuishwe katika mgao huo.

Alisema kutofunguliwa kwa akaunti ya pamoja baina ya manispaa hiyo na washirika wa mradi huo, kampuni hiyo imesababisha serikali kushindwa kufahamu kiasi cha fedha kinachokusanywa kila mwezi.

Rahma, alisema serikali kupitia Manispaa hiyo, imeshindwa kupokea mgao wa fedha zilizokusanywa katika kipindi hicho na kuathiri utoaji huduma bora kwa wananchi, zikiwemo usafi na mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

Alisema katika kipindi hicho, baraza hilo limetekeleza miradi ya maendeleo katika wadi. Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ufungaji wa taa 120 katika mitaa ya Kikwajuni, Rahaleo na Chumbuni kwa gharama ya Shilingi milioni 68. Kuhusu ujenzi wa jengo la biashara eneo la soko kongwe la kwa Haji Tumbo, Rahma, alisema umeanza kwa kuweka uzio.

Alisema baada ya kuweka uzio huo, ujenzi huo unaokadiriwa kugharimu shilingi 321,902,750 utaanza.

Alisema kati ya fedha hizo, shilingi 94,165,164,67 zimelipwa kwa mkandarasi kwa mujibu wa mkataba.

Akizungumzia kuhusu mradi wa maduka ya kisasa na migahawa ya Darajani Souk, alisema umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 5 zilizotolewa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na kampuni hiyo.



CARDI B
UKURASA 14





# TUMPONGEZE DIAMOND

WIKI iliyopita mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, ametoa burudani katika sherehe za utoaji tuzo za CAF zilizofanyika nchini Morocco.

Diamond amekuwa msanii wa kwanza kutoka Tanzania, kutoa burudani katika sherehe kubwa ya CAF, na hivyo ameweza kuonyesha nguvu yake katika sanaa.

Hata hivyo, shoo yake imeibua mjadala mkali baada ya kuwapo kwa maoni tofauti kwa mashabiki na wadau wa muziki nchini.

Wapo waliomponda kuwa amefanya vibaya na wengine wamempongeza kwa kupiga hatua licha ya shoo yake kuwa tofauti na walivyomzoea.

Shukuru Ombeni, ambaye ni mwalimu wa sanaa amesema shoo ya mwanamuziki huyo haikuwa mbaya kama wanavyosema watu, bali alitoa burudani kutokana na mazingira na watu waliokuwapo ukumbini.

Amesema kwa upande wake hakuona kitu kibaya wakati akitumbuiza katika hafla za kimataifa atakazoalikwa kutoa burudani.

"Watanzania lazima tujivunie msanii wetu kutumbuiza katika hafla kubwa kama ile, kwangu sijaona kosa lolote la kisanii amefanya, labda waseme aongeze ubunifu na kujiamini katika matukio makubwa kama haya," amesema Ombeni.

Ametoa ushauri wa Watanzania kujifunza kwa mataifa mengine yaliyoinuka katika sanaa, kwani msanii wao anapopanda jukwaani wanakuwa na kauli moja na kumuunga mkono, badala ya kumponda na kumuona kama hawezi.

BASI SAWA

## Mwijaku azidi kumbana Diamond



MSANII wa filamu, Mwijaku, ameendelea kumrushia maneno mwanamuziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, kuwa azidi kuwa mbunifu katika kulitawala jukwaa katika shoo za kimataifa.

Mwijaku amesema hawezi kufuta kauli yake ya awali kuwa hakufanya vizuri wakati akitumbuiza wakati wa sherehe za CAF za kutoa tuzo kwa wanasoka bora Afrika zilizofanyika nchini Morocco.

"Siwezi kutengua kauli yangu, nasisitiza Diamond hakufanya vizuri wakati alipotumbuiza, ukweli hakuimba licha ya kuingia na timu kubwa ya wachezaji," amesema.

## Isha eti unavuta skanka?



MWIMBAJI wa Taarab, Isha Mashauzi, amesema kuna baadhi ya watu wanadhani anavuta bhangi aina ya skanka, lakini hajawahi kutumia kilevi hicho katika maisha yake.

Akizungumza na EATV, Mashauzi amekiri kuwa kuna baadhi ya mastaa wanatumia aina hiyo ya kilevi ambacho kinawafanya watu kupata madhara mbalimbali ikiwamo kuchanganyikiwa akili.

"Watu wanasema kuna mastaa wanatumia skanka, hata mimi wanadhani natumia skanka, lakini sijawahi kugusa na nimewaacha waseme tu ukweli naujua mimi," amesema Mashauzi.



# ZUCHU AMSHANGAA YEMI ALADE

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, amesema katika kitu kilichomshangaza jinsi msanii wa Afrobeats wa Nigeria, Yemi Alade, hakumtoza pesa wakati alipoomba kufanya kolabo naye.

Akizungumza wakati akitangaza albamu yake mpya ya Money a Peace, amesema jambo hilo lilimshangaza kutokana na uzoefu wa wasanii wakubwa huwatoza pesa pale msanii mwingine anapotaka kufanya naye kazi.

"Yemi nilimtumia nyimbo mbili, lakini aliuchagua wimbo wa Lol Pop, sikuamini pale aliporudisha kiitikio kizuri sana na hakutaka hata senti moja jambo ambalo nilishangaa," amesema Zuchu.



# Kayumba alia na mapenzi

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Kayumba, amesema ameamua kuachana na mapenzi kutokana na kuteswa kila kukicha.

Akizungumza hivi karibu, amesema kabla ya kufanya uamuzi huo kila kukicha alibadilisha wanawake, lakini hakuna furaha aliyopata badala yake vurugu na mateso yalikuwa yakitawala.

"Nimekuwa nikiteswa katika mapenzi na ndio maana nyimbo zangu zimekuwa za kulia mapenzi tu. Siku moja niliambiwa sina hela hapo ndipo nikaamua kuacha kabisa mapenzi," amesema Kayumba.

FILAMU

# Muuza Mkaa, jini akakaa

**Na Adam Fungamwango**

LEO tutaiangalia filamu safi ya 'Muuza Mkaa' ambayo inaangalia mambo mbalimbali ya kijamii, ikiwamo ile dhana ya kuwapo kwa viumbe wasioonekana kwa macho ya kawaida, yaani majini.

Katika dunia hii, kitu kidogo kinaweza kutokea tu kwa bahati mbaya, lakini kikazusha mambo makubwa na ya kutisha kiasi cha kugofya watu, kufarakanisha watu na mengine yanayofanana na hayo.

Imechezwa na baadhi ya wasanii kama kina Hawa Mkwizu, Kassim Samwinzo, Ester Modekai, Abdul Shariff, Nasra Juma, Ibrahim Ally na wengineo.

Inaanza kuonyesha muuza mkaa akiwa amelala usingizi. Alikuwa kwenye eneo lake la kazi. Ghafla akaja dada mmoja, akamwamsha. Lakini wapi. Alipoona muuza mkaa amelala fofofo, akamimina mkaa kwenye chombo chake, na akachukua pesa na kuiweka mkononi mwa muuzaji. Hapo hapo aliamka. Akaanza kumfokea kuwa anaiba mkaa wake. Akamwambia mkaa aliochukua ni mwingi kuliko mkaa aliouweka. Akawa analalamika kuwa siku nyingi anapata hasara, kumbe ni mwanamke huyo. Wakati amemshika mkono akibishana, mara akapita mpenzi wake anaitwa Joyce.

Alipoona vile alidhani kuwa wapo kwenye mambo ya mapenzi. Ukazuka ugomvi mkubwa sana kati ya muuza mkaa wa mpenzi wake Joyce. Muuza mkaa alimtafuta yule dada ili akamweleze mpenzi wake kuwa wao siyo wapenzi, ila yalikuwa ni mambo ya kudaiana tu, lakini dada yule alikataa.

Kuna siku Joyce alikutana na yule dada aliyekuwa ameshikwa mkono na mpenzi wake, akamkoromea sana, lakini hakujibiwa kitu.

Shoga wa Joyce anajiwa na mwanamke mmoja ambaye anamtuma akamkanye shoga yake tabia ya kumkasirikia mpenzi wake na kusema yeye si mpenzi wa muuza mkaa. Lakini katika kuongea akawa anajigeuzageuza kuwa mtu wa ajabu, mara ana makucha makubwa, mara na macho makubwa kitu ambacho kilimtisha mwenzake.

Mwanamke huyo anakwenda kumhadithia Joyce na kumweleza kuwa yule msichana anayemtuhumu anatembea na mpenzi wake si binadamu wa kawaida, ila ni jini.

Joyce na mpenzi wake nao wanatokea kwa nyakati tofauti na staili ya kijini. Wote wanakutana sasa na kwenda kumuomba radhi mdada huyo ambaye ni jini.

Wanamkuta nyumbani kwake, lakini anashangaa kuwa hajawahi kwenda kununua mkaa, wala kukutana na mtu yoyote kati yao, hivyo anashangaa.

Kilichogundulika kuwa dada yule huwa anaingiwa na jini na kufanya mambo ambayo yeye hajui kama anafanya. Alifunga ndoa na jini mwanaume wakati akiwa usingizini bila yeye kujua na ndicho kinachomsumbua.



# MASTAA WA KIHINDI WANAOJUA KARATE

**Na Adam Fungamwango**

TANGU miaka ya 1970, Watanzania wamekuwa ni mashabiki wa filamu za Kihindi ambazo wamekuwa wapenzi wa kuzitazama hadi leo hii.

Tangu kipindi hicho kumekuwa na waigizaji au mastaa wengi ambao wanajulikana hata kwa majina, na wamekuwa wakipendwa na kukubalika kutokana na ubabe wao wanaouonyesha kwenye filamu zao.

Hata hivyo, si wote wenye uwezo wa sanaa za mapigano, badala yake wamekuwa na kazi kubwa ya kuigiza kupigana tofauti na wenzao ambao wamepitia mafunzo hayo.

Leo hii tutawaangalia nyota watano wa filamu za Kihindi ambao ni kweli wana ujuzi wa kupigana, hivyo katika kutokuwa na shughuli kubwa wanapoigiza picha.

Kumbuka kama staa yeyote hukumuona kwenye safu hii ambayo itaendelea tena wiki ijayo, basi ujue hao hawajui kupigana, ila wanaigiza tu.

**1# Mithun Chakraborty**

Sidhani kama kuna Mbongo yeyote toka kizazi cha 1970, hadi sasa ambaye hamfahamu staa huyo aliyecheza picha nyingi, lakini iliyomtambulisha na kumfanya kuwa nyota ni, 'Disco Dancer.'

Huyu ni mmoja wa waigizaji wa picha za mapigano mwenye mafunzo ya sanaa hiyo.

Ana mfunzo ya 'Aminal Style Kung Fu', yaliyomfanya kupata mkanda mweusi.

**2# Akshay Kumar**

Huyu jamaa ambaye ni mbabe kweli kweli ana mikanda miwili myeusi ya mapigano ya 'Shotokan Karate na Muay Thai, hivyo ukimuona kwenye picha zake usidhani anaigiza tu hivi hivi, anajua kweli kupigana, hivyo kumrahisisha kazi kwenye kazi yake.

**3# Suniel Shetty**

Huyu jamaa ni swahiba yake sana Akshay Kumar. Kuna picha nyingi sana hawa jamaa wamecheza pamoja.

Kumbe moja kati ya sababu ni kwamba wote hawa wanajua kupigana kweli kweli.

Sifa yake huyu ni ana mkanda mweusi wa mapigano ya judo, pia ameshawahi kucheza 'kick boxer.'

Ndiyo maana jana huwa harembi, ukimzingua tu anakuzingua, wala hacheleweshi wala kuchekacheka.

**4# Govinda**

Jamaa huyo naye siyo mzembe mzembe, anajua kupigana kweli. Amejifunza sanaa chache za mapigano, ingawa hadi sasa hana mkanda hata mmoja.

Sababu ni kwamba amepigana au kujifunza sanaa za mapigano tofauti tofauti, hivyo hajawahi kukaa kwenye staili moja akawa nguli. Yeye alitaka kila staili ajifunze, hivyo akajikuta akigusa kila eneo na kuondoka, hivyo hakuna sehemu aliyefika mwisho na kutunikiwa mkanda. Inaonekana alijifunza kwa ajili ya kupata urahisi kwenye kuigiza tu na si kumuliki mikanda.

**5# Ajay Devgan**



Staa huyu na filamu za Kihindi ni moja kati ya waigizaji watata, na ukweli ni kwamba yeye pia ana ujuzi kwenye sanaa za mapigano.

Ana mkanda mweusi wa 'Tae Kwon Do', ambayo inamfanya kuwa rahisi sana kwake kuigiza.




# Cardi B yamkuta

RAPA mkali wa Marekani, Cardi B, amejikuta akikabiliwa na ukosoaji baada ya kujiita yeye ni mrembo na asiyeyumbishwa na wanaume.

Katika ujumbe wake kupitia ukurasa wake wa X, Cardi B, Cardi B aliorodhesha kile anachoamini kuwa yeye ana sifa zote za kuitwa shupavu ikiwamo umbo lake, uso, ari ya kusisimua na mwili wake wenye harufu nzuri.

Kufuatia ujumbe huo, wafuasi wake walimiminika mtandaoni na kumshutumu kuwa ana ubinafsi na kwamba muktadha wake unatoa mafunzo hasi kwa wanawake.



## Tiwa Savage kanunua nyumba London

MKALI wa muziki wa Afrobeats, Tiwa Savage, ametangaza furaha yake baada ya kununua nyumba yake mwenyewe katika jiji la London, nchini Uingereza.

Tiwa Savage kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameweka video ikionyesha nyumba ya ghorofa moja yenye vyumba vitatu.

"Nilinunua nyumba yangu ya vyumba vitatu katika jiji la London mwaka jana na hatimaye sasa iko tayari," amesema Tiwa Savage.


Baada ya ujumbe huo kuchapishwa, wafuasi wake walishiriki kwa kutoa maoni mbalimbali, wengi wakimpongeza kwa kufikia hatua hiyo ya kimaendeleo.

## Adekunle utabaki peke yako

MWIMBAJI wa Afrobeats kutoka Nigeria, Adekunle Gold, ameibua gumzo baada ya kueleza maisha nchini humo yanazidi kuwa mabaya.

Akitumia ukurasa wake wa X, Adekunle amewashauri Wanigeria wenzake kulinda mapenzi yao, kwa sababu nchi hiyo inazidi kudhoofika.

"Kuna kitu kuhusu mahali hapa ambacho kinadhoofisha ubora maisha. Kujitahidi hapa ni kazi bure, kwani mazingira yanakuvuta chini mpaka uwe kama watu wengine," amesema.





## Tems hataki shida

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, Tems, ametoa siri kwa nini hapendi kutumia simu janja katika maisha yake.

Akifanya mahojiano na jarida la Glamour la Ujerumani, amesema hata yeye hajui kwa nini hana mapenzi na simu, hivyo anatafuta njia ya kuachana nayo.

"Sipendi simu yangu mahiri hata hivyo. Napendelea kuishi duniani na kuwa na uzoefu. Nikiwa na kisingizio kidogo cha kuacha simu yangu kwenye droo, nitaipokea kila wakati. Ningesema. kwamba ni usimamizi wangu na familia yangu ndio huniweka msingi haswa familia yangu, mama yangu na kaka yangu.

## Timi asimulia yaliyomkuta

MWANAMUZIKI wa Nigeria Timi Dakolo, mwanamke aliyekutana naye ndani ya kanisa, sasa amekuwa mke wake.

Akisimulia namna alivyokutana kwa mara ya kwanza na mke wake Busola, amesema siku hiyo alimuona katika hafla moja kanisani akiwa amekunja uso, lakini alijipa moyo kwamba huyo ndiye mke wake mtarajiwa.

"Baada ya hapo kila Jumapili nilimtafuta sehemu moja na akaniambia simu yake iliibiwa. Tukawa marafiki na sikumwambia kile cha moyoni mwangu na yeye alitaka tuwe marafiki tu tuliendelea kuongea na niliteseka mkononi mwake,"amesema.





# Rushwa Minjingu funga kazi, Kamishna TRA aambiwa

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

WAFANYABIASHARA mkoani Manyara wamemwomba Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda kuwadhibiti baadhi ya watumishi kwa kuomba rushwa kwenye vizuizi ili kuvusha bidhaa zao.

Ombi hilo walilitoa jana mjini hapa, wakati wakizungumza na Kamishna Mwenda.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Manyara, Musa Msuya, alidai licha ya mazingira mazuri yaliyowekwa na serikali ya awamu ya sita kufanya biashara, kuna tatizo kwenye kizuizi cha Minjingu kwa wao kuombwa rushwa ili kuruhusiwa kuvusha bidhaa zao.

"Tukiagiza mizigo Arusha haivuki Makuyuni, tunalazimishwa kutoa rushwa, ni lazima uandae Shilingi 200,000 za kuhonga ili kuruhusu mzigo utoke," alidai Msuya.

Aliendelea kudai kuwa kuna wakati aliagiza bidhaa Arusha, gari lake lilikamatwa na kuzuiwa kwa saa zaidi ya 10 na watumishi hao na kukubali kutoa rushwa ili liachiwe.

Licha ya vikwazo hivyo, awali alisema malalamiko mengi dhidi ya TRA yanatatuliwa kwa wakati na wanalipa kodi bila kutumika mtutu wa bunduki.

"Zamani tulikuwa tunakusanya kodi kama vile tuko vitani na watumishi wa TRA, tulikuwa hatuwezi kukaa nao hata kunywa soda," alisema Msuya.

Mfanyabiashara mwingine, Abeid Baiday, alidai rushwa inayotajwa Makuyuni na Minjingu ipo kizuizi cha Katesh na kwamba iliyopo Minjingu ndio funga kazi.

Baiday, alidai gari linashikiliwa bila kosa mpaka liachiwe mtu anatakiwa atoe rushwa.

"Mimi pale Minjingu natamani niende na fimbo niwachape viboko maana wamezidi kwa rushwa," aldai.

> **"Zamani tulikuwa tunakusanya kodi kama vile tuko vitani na watumishi wa TRA, tulikuwa hatuwezi kukaa nao hata kunywa soda," alisema Msuya.**

Akijibu madai ya wafanyabiashara hao, Mwenda alisisitiza kuwa watumishi wa TRA wanalipwa mishahara na serikali na wapo kuwahudumia wafanyabiashara na siyo kuwaomba rushwa.

Aliwataka wafanyabiashara wasikubali kutoa rushwa kwa watumishi hao na kuchukua ushahidi kisha kuwaripoti kwa wakuu wao wa kazi ili hatua kali zichukuliwe dhidi yao.

Alisema ametoa maelekezo kwa Meneja wa Mamlaka hiyo wa mkoa kushughulikia madai hayo dhidi ya watumishi hao ili hatua zichukuliwe dhidi yao na kuwaondolea kero wafanyabiashara kwenye vizuizi hivyo.

Alisema tuhuma hizo za rushwa ni miongoni mwa vigezo ambavyo meneja wa mkoa wa TRA anapimwa kwenye utendaji ni kuzalisha biashara nyingi na siyo kuua biashara.

Kuhusu wafanyabiashara kukaguliwa hesabu za miaka 10 iliyopita, alisema walikubaliana iwe ndani ya miaka mitatu.

Vilevile Mwenda, aliwataka wafanyabiashara wenye matatizo ya kulipa kodi kukutana na meneja wa mamlaka hiyo kukubaliana kulipa kwa awamu bila usumbufu.

Kamishna huyo wa TRA, alitembelea Kampuni ya Mati Super Brands Limited na kuipatia tuzo ya heshima baada ya kulipa kodi Sh. bilioni tano kwa miezi mitano.

Alisema wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa kampuni hiyo ili kufikia malengo yake kwa kuwa ni mlipakodi mkubwa wa kitaifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, David Mulokozi, aliipongeza TRA kwa kuwapatia ushirikiano na kukua kwa kasi na kusambaza bidhaa zao mpaka nje ya nchi.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Fani Mussa, akisoma taarifa katika kikao cha maandalizi ya mpango kabambe wa afya kwa mwaka wa 2025/2026 jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wafugaji: Hatari kuendelea kuishi Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,**
NGORONGORO

WAFUGAJI 97 wa jamii ya Kimasai, waliokubali kuhama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wametoa angalizo kwa waliobaki kuwa ni hatari kuishi na wanyama wakali katika eneo moja.

Mwitikio uliopo sasa wa wananchi kukubali kuhama Ngorongoro, kupisha shughuli za uhifadhi, umesaidia kupunguza shughuli za kibinadamu hifadhini, kukosa uhuru wa kumiliki vyombo vya moto, kufanya shughuli za kiuchumi na uhuru wa kutembea ndani ya hifadhi baada ya saa 12 jioni.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wafugaji hao, akiwamo Daudi Melubo, Mkazi wa Kijiji cha Kayapus, alisema ameamua kuondoka kwa hiari kwenda Kijiji cha Msomera Kata ya Misima Wilaya ya Handeni mkoani Tanga ili yeye na familia yake kupata uhuru nje ya Ngorongoro.

Melubo na wenzake, sasa wanakuwa kundi la 21 la awamu ya pili lenye kaya 23, watu 97 na mifugo 196 kuhama ndani ya hifadhi hiyo kuelekea Msomera na maeneo mengine waliyochagua wenyewe.

Mbali na Msomera, Saunyi (Kilindi), wananchi wengine wamehamia Wilaya za Monduli (Arusha), Meatu (Simiyu) na Simanjiro (Manyara).

"Nimeamua kuhama kwa hiyari yangu kwenda Msomera kwa sababu huko kuna uhuru wa kujiendeleza, nitajenga nyumba, nitamiliki ardhi, watoto wangu wataenda shule bila hofu ya mnyama mkali na hakuna sheria kama hifadhini," alisema. Naishiye Sembeta alisema kuwa: "Sisi wanawake tumekuwa tukitembea umbali mrefu kwenda kutafuta kuni porini huku tukihatarisha maisha yetu, ila sasa tunahamia Msomera na tunaamini maisha yetu yatabadilika na kuwa bora zaidi."

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa zoezi hilo, Meneja wa Mradi, Ofisa Uhifadhi Mkuu wa NCAA, Florah Assey, alisema hadi kufikia Desemba 19, mwaka huu, kaya 1,678 zenye watu 10,073 na mifugo 40,593 zimehama ndani ya hifadhi hiyo kuelekea Msomera na wengine maeneo waliyochagua wenyewe.

Kwa mujibu wa Florah, utaratibu uliopo ni kuhakikisha kuwa zoezi la uandikishaji, tathmini ya maendelezo na uhamishaji vinaenda sambamba ili kila mwananchi atumie muda mfupi kuhama ndani ya hifadhi hiyo na kwenda eneo alilochagua.

## Watakiwa kuzingatia sheria ugavi, manunuzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATAALAMU wa ununuzi na ugavi wametakiwa kuzingatia sheria za manunuzi na kutumia mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (NeST) ili kuongeza uwazi na ubora katika miradi ya serikali.

Wataalamu hao pia wameonywa kujiepusha na rushwa kwa kuwa vitendo hivyo vitachelewesha ununuzi na kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuiingizia serikali hasara ya mabilioni ya fedha. Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, alisema hayo jana jijini Arusha, wakati akifunga Kongamano la 15 la Wataalamu wa Bodi ya Ununuzi na Ugavi (PSPTB) lenye kauli mbinu ya mabadiliko ya ununuzi na ugavi kwa usimamizi bora wa rasilimali na kuhudhuriwa na washiriki 1,900. "Katika siku tatu za kongamano hili mmepata fursa ya kujifunza, kubadilidilishana uzoefu na kuweka mikakati kusadia sekta ya ununuzi na ugavi na kuwa na tija kwa taifa. Hivyo mnapotoka hapa nendeni mkawe chachu ya mabadiliko chanya katika maeneo yenu ya kazi kwa kukata rushwa na kutumia NeST kuongeza ufanisi wa miradi," alisema Musa.

Alisema kongamano hilo limeazimia kupunguza changamoto zilizopo kwenye fani ya ununuzi na ugavi nchini. "Ni vema yakapewa nafasi ya kutosha katika maeneo yenu ili kufikia malengo ya serikali yaliyokusudiwa, lakini pia yakawe dira ya kuwaongeza katika majukumu yenu ya kila siku," alisema.

Alitoa mfano kuwa Mkoa wa Arusha kwa kipindi cha mwaka mmoja umepokea fedha zaidi ya Sh. trilioni 2.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alisema endapo wataalamu hao hawatatimiza wajibu wao, miradi hiyo haiwezi kutekelezwa kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

"Naomba hakikisheni mnatoa huduma bora kwa Watanzania kwa kuzingatia ununuzi wa thamani ya fedha iliyotolewa.

"Ninawaomba mkatoe huduma bora kwa Watanzania kwa kuzingatia ununuzi wa thamani ya pesa iliyotolewa ionekane kwenye miradi hiyo". Kwa upande mwingine, aliwataka wataalamu hao kuepuka adhabu zisizo za lazima, huku akiwasisitiza waajiri kutenga fedha za kuwajenga uwezo ili waendelee kutekeleza majukumu yao kitaalamu zaidi. Makamu Mwenyekiti Bodi Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Benezeth Ruta aliwasisitiza wataalamu hao kuheshimu na kuzingatia sheria za ununuzi na ugavi ili nchi iweze kufikia malengo ya uchumi yanayokusudiwa. "Kongamano letu lilijielekeza kujadili mabadiliko ya kidijitali kwa maendeleo endelevu ya taifa. Ninawaomba mkazingatia maadili na kutanguliza uzalendo mbele kwa kuwa sekta hii ni injini ya nchi kutekeleza miradi ya maendeleo," alisema.



# Vijana, watoto zamani 'walivyoinjoi' Krismasi zao

Na Adam Fungamwango

JUMATANO ijayo, waumini wa Kikristo wote ulimwenguni wataungana na wenzao duniani kusherehekea sikukuu ya Krismasi, ambayo kwa jina lingine huitwa Noel.

Ni sikukuu inayosherehekewa Desemba 25 ya kila mwaka kuadhimisha kuzaliwa na Masiya, Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita kwenye mji ya Bethlehemu, nchini Israel.

Hii ni moja ya sikukuu maarufu zaidi duniani, ambapo hapa nchini huwa tunaona wazazi wakiwa bize kuwanunuliwa mahitaji watoto wao na kuhakikisha wanakula vizuri, kabla ya kwenda Kanisani kumshukuru Mungu, lakini baada ya hapo hugawanyika, wakubwa wanakwenda sehemu zao kwa ajili ya kuburudika na kusherehekea, pia watoto nao huelekea sehemu zao ambazo nazo huzipenda kwenda na watoto wenzao.

Wakati wakubwa hupenda kwenda sehemu zenye vinywaji na nyama choma, na burudani ya muziki, watoto wa kizazi cha sasa hupenda kwenda sehemu kama vile baharini 'bichi', au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya watoto kama vile kubembea, kuendesha farasi wa umeme na mengine mengi.

Haya ni kwa wazazi na watoto wa kisasa. Miaka ya nyuma, maandalizi ya sikukuu hii yalikuwa tofauti na sasa. Yalikuwa makubwa zaidi na yaliyochukua muda mrefu kuliko sasa. Yalikuwa na pilikapilika nyingi kuliko sasa kwa wazazi na watoto pia.

Siku hizi baba anaweza kupata pesa na kununulia watoto nguo wakati mwingine bila hata wao kujua. Wanashtukia zimeletwa tu. Kutokana na teknolojia kuwa ndogo, uhaba bidhaa kama nguo, viatu na vitu vingine vilisababisha kuwe na pilikapilika za aina yake.

Kwanza kabisa watoto wa siku hizi wana nguo nyingi nzuri kiasi kwamba hata akinunuliwa mpya, zinakuwa hazina sana tofauti na alizonazo.

Zamani kwenye sikukuu kama hii picha linaanza kwanza kwenye redio. Hakukuwa na redio yoyote zaidi ya RTD, hivyo nyimbo za Krismasi zikianza kupigwa tangu tarehe 15, wote mtasikiliza na kila mtu atajua sikukuu inakuja, hivyo inaleta msisimko mno, tofauti na sasa ambapo kuna baadhi ya vituo ambavyo havilazimiki kupiga nyimbo hizo.

Pia watoto na vijana wa sasa si wasililizaji sana wa redio, zaidi ya televisheni na simu za mkononi ambapo husikiliza nyimbo wanazozitaka wao tu.

Kwa miaka ya karibuni hata miti halisi ya kupamba Krismasi haipo, badala yake ipo ya kutengenezwa ambayo si halisi. Hii imekuja kuua sana biashara ya miti halisi.

Siku chache kabla ya Krismasi, baba atawapeleka kwa fundi cherehani kupima suruali, au gauni, wakati huo tayari vitambaa vimeshanunuliwa hasa wale wa vijijini. Wengine hupelekwa mjini kununuliwa gauni, shati, suruali na viatu.

Wazazi wakati huo walilazimika kuwachukua watoto wao kwenda nao mjini kwa sababu ya kujaribu nguo na viatu kwani isingewezekana kurudisha au kuanza kuirekebisha kwa fundi.

Kulikuwa maduka maalum ya kununua nguo za si kwa machinga kama sasa, lakini viatu hasa vya sikukuu na shule vilikuwa vinanunuliwa kwenye kampuni ya viatu Bora.

Na kama mtoto hatochukuliwa kupelekwa mjini kukuliwa viatu, basi litachukuliwa katarasi ngumu au boksi, atalikanyaga, huku kalamu ikizungushwa kwa kuchorwa kuzunguka mguu, ili atakapoenda mjini basi viatu vitakachowekwa na kuwa sawa na mzunguko huo ulioko kwenye boksi au karatasi ngumu, vitakuwa vinamtosha mhusika na kweli ilikuwa hivyo.

Ilikuwa ni wiki ngumu kwa watoto wa zamani kuelekea kwenye sikukuu. Tena usiombee nguo zinunuliwe mapema. Ni kwamba kila mara atakuwa anakwenda kufungua sanduku na kuziangalia. Wakati mwingine atazijaribu na kuzirudisha akiombea sikukuu ifike upesi, avae akawaringishie wenzake ambao ana uhakika nao watakuwa na nguo mpya pia. Hapo sasa ni mashindano ya nani kapendeza zaidi ya mwingine.

Ukweli ni kwamba wazazi wa sasa wako karibu zaidi na familia zao hasa siku za sikukukuu mtu anaweza kutoka yeye mkewe na watoto, wakaenda popote pale kwa ajili ya kusherehekea, tofauti na zamani ambapo baba hakuwa na muda wa eti kuondoka akiwa ameongozana na watoto wake.

Kinababa wa enzi hizo wao walikuwa wanakwenda kivyao, kwenda kukutana wenyewe wanaume sehemu zao za burudani, hakuna mtoto yoyote anayetakiwa hapo.

Akinamama nao walikwenda sehemu zao wakiwa na watoto wenye umri mtoto mchanga hadi sita, na wale kuanzia miaka saba hadi 18 nao hawakutaka kuongozana na watoto, baba au mama. Hawa nao walikwenda sehemu zao. Hawa ndiyo asilimia kubwa ndiyo waenda 'bichi' au kule vijijini 'pikniki'.

Kwa miaka ya hivi karibuni pia kumekuwa na upungufu mkubwa wa maeneo ya watoto kwenda kusherehekea sikukuu kuliko wakubwa.

Mabaa, mahoteli, kumbi za burudani kwa wakubwa zimejaa tele, lakini watoto wamesahaulika.

Hakuna maeneo ya wazi kama zamani yalikuwa yakimilikiwa na Jiji yenye bustani ambayo yatawafanya watoto kwenda kufurahia sikukuu. Kuna maeneo machache sana yaliyobaki baada ya mengi kupigwa bei, ambayo watoto hukusanyika na kupata burudani.

Zamani kulikuwa na meneo mengi ya wazi ambayo yalitengenezwa kama vizimba kwa kutumia magunia, na wakawa wanaingia na pesa, humo wanakuta ngoma za asili, maigizo, na michezo mbalimbali ya watoto kama kubembea, huku kukiwa pia na vyakula mbalimbali kama mishikaki, mihogo, Ice Cream na vingine vingi ambavyo watoto walifurahia sana.

Kukosekana maeneo ya burudani kwa watoto ndiyo imesababisha miaka ya hivi karibuni watoto nao kutinga kwenye kumbi za starehe, licha ya kwamba hawaendi kustarehe, lakini wanatumia majengo hayo ambayo kiafya kwao si mazuri. Wanakuwa wengi na kunakuwa na joto kali, hivyo wakati mwingine yanatokea matatizo makubwa. Kwenye miaka ya karibuni kumetokea maafa watoto walifariki kwenye ukumbi uliokuwa na joto.

Hii imesababisha hata Makamanda wa Polisi wa Mikoani kila mwaka kupiga marufuku 'disco toto', au watoto kuingia kwenye kumbi.

Ni hatari kubwa watoto kuingia kwenye kumbi ambazo zimefunikwa juu, lakini hili lingeepukika kama nchi ingekuwa na maeneo mengi ya wazi kama zamani kwa ajili ya watoto nao kuinjoi sikukuu kama wenzao wa zamani.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Rais Tshisekedi amtimua kazini mkuu wa majeshi

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amemwondoa madarakani mkuu wa majeshi na maofisa wengine wa kijeshi.

Mabadiliko hayo katika jeshi yamefanyika hivi karibuni na kuibua hisia tofauti kwa wananchi.

Katika taarifa ya Rais Tshisekedi iliyosomwa kupitia kituo cha televisheni ya taifa, haikueleza sababu ya kuondolewa kwa mkuu wa majeshi Christian Tshiwewe Songesha, na nafasi yake kuteuliwa Luteni Jenerali, Jules Banza Mwilambwe.

Wataalamu wa masuala ya ulinzi wanaamini kuteuliwa kwa Luteni Jenerali Mwilambwe ambaye anatokea kwenye kikosi cha ulinzi wa rais, huenda kutokana na kukosa mafanikio kwenye vita vinavyoendelea mashariki mwa nchi hiyo kwa zaidi ya miaka miwili.

Hata hivyo, wengine wanadhani kwamba mabadiliko hayo yanahitajika kuanzia ngazi za chini na kupanda juu.

Patrick Mundeke, ambaye ni mwanasiasa na pia mchambuzi wa masuala ya ulinzi alieleza katika mabigano ya muda mrefu lazima kuwepo kwa maboresho ndani ya jeshi.

"Ili kuweka sawa kwenye uwanja wa mapigano, lazima kuweko na maboresho katika hali ya maisha ya wanajeshi na uongozi wa jeshi wenye watu wazoefu," alisema Mundeke.

Kwa upande wake Marrion Ngavo, mwenyekiti wa mashirika ya kiraia katika mji wa Goma, alipongeza mabadiliko hayo ya kijeshi, huku akiwaomba viongozi hao wapya wa jeshi, kuyarejesha chini ya udhibiti wa jeshi la serikali maeneo yaliyotekwa na waasi wa AFC-M23.

Wakati huo huo, jopo la kimataifa la nchi za ukanda wa maziwa makuu, linaloongozwa na Uholanzi, limetangaza kusikitishwa kwake kufuatia kusuasua kwa mazungumzo ya kuleta amani kati ya DRC na Rwanda.

Katika tamko lao la pamoja lililotolewa juzi, jopo hilo liliwaomba viongozi wa nchi hizo mbili kurudi kwenye meza ya mazungumzo, ili kufanikisha amani ya kudumu katika mkoa wa Kivu Kaskazini ambao umegeuka kuwa uwanja wa mapigano.

Aidha jopo hilo lenye wajumbe kutoka Ubelgiji, Umoja wa Ulaya, Ufaransa, Ujerumani, Uholanzi, Sweden, Uswisi, Uingereza na Marekani, lilimpongeza Rais wa Angola João Lourenço, kwa jitihada zake za kutafuta amani katika taifa hilo.

***DW***



Waandamanaji wakiwakimbia polisi wakati wa purukushani za kudhibiti maandamano katika Kitongoji cha Luis Cabral katika Jiji la Maputo, Msumbiji, wiki iliyopita. **PICHA: REUTERS**

# Macron kuendelea kubaki Mayotte

**PARIS,** UFARANSA

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amerefusha ziara yake katika kisiwa cha Mayotte, baada ya kushuhudia hali mbaya kutokana na kimbunga Chido.

Kiongozi huyo alikumbana na hasira za wananchi wa kisiwa hicho kufuatia kuishi katika mazingira mabaya na kukata tamaa kutokana na ukubwa wa madhara.

Wananchi hao walimlalamikia Rais Macron, jinsi wanavyoishi bila chakula na maji mara alipotembelea kisiwa hicho ambacho kipo Bahari ya Hindi.

Rais Macron, aliwasili siku tano baada ya kimbunga Chido kukipiga kisiwa hicho na kusababisha uharibifu mkubwa ambao haujawahi kutokea.

"Kwanza kabisa nataka kuwaambieni kuwa najua mmekuwa na wakati mgumu katika siku sita zilizopita. Hofu kutokana na hiki kimbunga. Sikuhusika kwa vyovyote na kimbunga hicho. Mnaweza kunilaumu, lakini haikuwa mimi," rais Macron alijitetea.

Timu za uokoaji zinaendelea kuwatafuta manusura na kugawa misaada ya dharura.

Idadi ya awali iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ufaransa inaonyesha kuwa watu 31 wamethibitishwa kufa na wengine 2,500 kujeruhiwa.

***DW***

## Msumbiji yajiandaa kwa maandamano

**MAPUTO,** MSUMBIJI

TAIFA la Msumbiji linajiandaa kukabiliana na maandamano ya wafuasi wa vyama vya upinzani, wakati Tume ya Uchaguzi inatarajia kutangaza matokeo ya mwisho ya uchaguzi Jumatatu.

Kiongozi wa upinzani, Venancio Mondlane, ametishia kuitisha maandamano yenye vurugu nchi nzima kama Baraza la Kikatiba litaidhinisha matokeo ya awali ambayo yalimtangaza mgombea wa chama tawala cha Frelimo, kuwa mshindi.

Baada ya matokeo hayo, Msumbiji imekumbwa na ghasia kwa kipindi cha miezi miwili na kusababisha vifo vya watu 130, pamoja na uharibifu wa mali.

Aidha, vurugu hizo zimekwamisha shughuli za kibiashara na kuathiri uzalishaji viwandani.

Aidha, Marekani ilitangaza hali ya tahadhari kwa raia wake na kuonya dhidi ya safari za kwenda Msumbiji, ikisema maandamano yanaweza kugeuka haraka na kuwa fujo.

***DW***

## Poland yasogeza mfumo wa kujilinda mpakani

**WARSOW,** POLAND

POLAND imetangaza kupeleka mfumo wa ulinzi wa anga wa NASAMS katika mpaka wake na Ukraine kwa ajili ya kujilinda dhidi ya makombora ya Russia.

Hata hivyo, wanajeshi 100 wa Norway waliwasili katika eneo hilo kama ujumbe wa NATO kwa ajili ya kulinda kituo cha anga cha Rzeszow ambacho kipo karibu na mpaka wa Ukraine.

Ujumbe uliochapishwa kwenye mtandao wa X ambao (zamani ulijulikana kama Twitter) ulisema kuwa kituo cha Rzeszow, ambacho ni kitovu cha usafirishaji misaada kutoka nchi za Magharibi kwenda Ukraine, kitalindwa na wapiganaji wa F-35.

Jeshi la Poland lilisema kuwa misheni hiyo inatarajiwa kudumu hadi kipindi cha sikukuu ya Pasaka.

Mfumo wa hali ya juu wa ulinzi wa anga wa Norway umewekwa kuzuia makombora yanayorushwa kwa umbali mdogo na wa kati katika hali zote za hali ya hewa.

Mfumo huo ulitengenezwa na kampuni ya Norway ya Kongsberg pamoja na kampuni ya Marekani ya Raytheon tayari unatumiwa na jeshi la Ukraine.

Ukraine imetoa wito kwa washirika wake wa Magharibi kuangusha makombora na ndege zisizo na rubani za Russia ikiwa zitaruka juu ya eneo la NATO au hata karibu na mipaka ya magharibi ya Ukraine.

Hata hivyo, maofisa wa NATO wamekuwa wakisema hilo suala haliwezekani.



Mamalishe akiandaa biashara zake katika mazingira ambayo ni hatari kwa afya za wateja wake, kama alivyonaswa na kamera yetu eneo la Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ajifungua watoto wanne, apata tatizo la upumuaji

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

MKAZI wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Raina Mathew (34), amejifungua watoto wanne katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera Bukoba (BRRH) na kupewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani Kanda, Bugando kwa ajili ya uangalizi zaidi.

Mama huyo ambaye pia ni mke wa mwandishi wa habari mkoani hapa, Benson Eustace, alijifungua pacha hao wiki mbili zilizopita kisha kupewa rufani kutokana na tatizo la upumuaji na sasa anaendelea na kliniki baada ya kuruhusiwa.

Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Dk. Mike Mabimbi alisema mama huyo baada ya kujifungua, alipatiwa rufani kutokana na tatizo la kupumua alilolipata wakati wa kujifungua.

Alisema watoto hao wanaendelea kupewa uangalizi kutokana na kuzaliwa chini ya uzito wa kilo 1.5 badala ya kilo 2.5 zinazohitajika.

"Kwa sasa maendeleo yao ni mazuri. Wameanza kuongezeka uzito na wanapata huduma stahiki kama watoto wengine waliopo hospitalini hapa. Angalizo letu ni kwamba pindi watakaporuhusiwa kwenda nyumbani wasianze kutembelewa na watu kuwaangalia mpaka pale tutakapotoa ruhusa," alisema Dk. Mabimbi.

Alisema kitendo cha kuwepo kwa mwingiliano wa watu pindi wanaporudi nyumbani kinasababisha kuongezeka kwa athari na maradhi kwa watoto hao.

Ofisa Lishe, Victoria Ngatunga, alisisitiza umuhimu wa lishe yenye virutubisho vingi kwa kina mama wanaonyonyesha, akiwashauri kula mara kwa mara, huku akizingatia vyakula vya kimiminika ili kuchochea uzalishaji mwingi wa maziwa.

Akizungumza na Nipashe, baba wa watoto hao, Eustace, alisema mke wake alijifungua watoto wanne, wawili wakike na wawili wa kiume na mpaka sasa wanaendelea kupata huduma hospitalini hapo wakisubiri hali zao kutengamaa.

Eustace alisema kliniki hiyo ni kwa ajili ya uangalizi ambako alirudi juzi na kufanyiwa vipimo, kisha kuruhusiwa na kutakiwa kurudi tena Januari 20, mwakani.

**Mama huyo ambaye pia ni mke wa mwandishi wa habari mkoani hapa, Benson Eustace, alijifungua pacha hao wiki mbili zilizopita kisha kupewa rufani kutokana na tatizo la upumuaji na sasa anaendelea na kliniki baada ya kuruhusiwa.**

Alisema watoto bado wanaendelea kupatiwa huduma na kuwa tayari wametoka kwenye hatua ya uatamizi (incubation) na sasa wameanza kuwakumbatia ambako walihitajika ndugu kwa ajili ya kusaidia huduma hiyo.

"Kikubwa ambacho tumeambiwa na madaktari ni kuhakikisha watoto wanapata maziwa na kwa sasa wanaendelea vizuri na mambo mengine yapo ndani ya uwezo wa madaktari," alisema.

Mkuu wa Mkoa Kagera, Fatma Mwassa akizungumza alipotembelea watoto hao kuwajulia hali, aliwapongeza madaktari na wauguzi wa hospitali hiyo kwa jinsi wanavyoendelea kuwapa huduma bora kuwanusuru pacha hao na kuhakikisha wanarejea katika hali yao ya kawaida.

Alisema watoto hao wanaoendelea kupatiwa huduma na uangalizi hopitalini hapo na wataalamu mbalimbali mpaka pale watakapokuwa katika hali yao ya kawaida na mama yao kuwa tayari kuwahudumia.

# PPP kuimarisha utekelezaji miradi mikubwa

**Na mwandishi Wetu,** DODOMA

WATAALAMU wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi nchini wameagizwa kuhakikisha miradi yote mikubwa yenye mvuto wa kibiashara inatekelezwa kwa njia ya ubia baina ya pande hizo (PPP) ili kuipunguzia serikali mzigo wa gharama.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, alisema hayo juzi kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Natu Elmaamry Mwamba, wakati akifungua kikao cha kuimarisha ushirikiano kati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania kuhusu PPP.

Iisema utekelezaji wa miradi kupitia PPP ni sehemu ya kujenga uchumi imara na ni suala ambalo linatekelezwa na nchi nyingi duniani.

"Msiogope, hata nchi zilizoendelea zinatekeleza miradi yao kupitia PPP, ukiangalia madaraja na majengo mbalimbali wameyatekeleza kupitia PPP. Sekta binafsi wakipewa nafasi wanafanya vizuri", alibainisha.

Omolo aliwaagiza wataalamu hao kukuza uelewa wa dhana ya PPP kwa wadau mbalimbali kwa kuwa bado kuna changamoto ya uelewa kuhusu suala hilo na faida zake.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Rashid Ali Salim, aliwaagiza wataalamu hao kuhakikisha wanayafanyia kazi yale yote waliyokubaliana katika kikao hicho hususani kuwa na mkakati wa pamoja wa kuuza fursa na kuibua miradi ya PPP.

Naye Kaimu Kamishna wa PPP, Wizara ya Fedha, Bashiru Taratibu, alisema katika kikao hicho kuna masuala mbalimbali wameazimia kuyatekeleza ikiwamo maboresho ya sheria ili kurahisisha shughuli za PPP nchini hususani katika kutekeleza miradi ya pamoja katika ya Zanzibar na Tanzania Bara.

"Tumejadili kuhusu miradi ya pamoja ambayo Sekta Binafsi inaweza kutekeleza kama mradi wa Daraja la Dar es Salaam hadi Zanzibar lakini kila sehemu wana sheria yao ya PPP, kwa hiyo tumekaa kuona namna bora ya kutekeleza suala hilo iwapo mwekezaji atajitokeza", alisema.

Alisema Tanzania inahitaji kuwa na sera au sheria ya PPP inayoelezea utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuwa suala kama hilo limeshajitokeza katika nchi za Afrika Mashariki na kuna miradi ambayo inaunganisha nchi moja na nyingine na kwa sasa tayari kumeshaandaliwa Sera ya PPP ya Afrika Mashariki.

Kamishna wa Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC), David Kafulila, alisema katika kikao hicho wamejadiliana mambo mbalimbali ya kurahisisha ubia nchini ili kuipunguzia mzigo serikali wa kugharamia miradi ya maendeleo ambayo inaweza kugharamiwa kupitia PPP.

Alisema Tanzania kwa sasa inafanya vizuri katika eneo la PPP na kwamba kwa Tanzania Bara, kuna takribani miradi 74 ambayo iko katika hatua za mwisho kuanza kutekelezwa na Zanzibar kuna takribani miradi 13.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-44

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"Waooo jamani karibu shemeji." Teddy akamlaki mgeni wake ambaye alimpigia simu kuwa atafika majira ya saa tano asubuhi siku ya Jumamosi hiyo.

Hakwenda kazini siku hiyo, ilikuwa siku yake mapumziko. Alikuwa ameanza kazi miezi mitatu iliyopita kwenye Hospitali ya Amana, Dar es Salaam, hivyo aliondoka kwa mama yake mkubwa alikokuwa amekaa na sasa alikuwa amepanga Chang'ombe Maduka Mawili.

Akamkumbatia na kumuingiza sebuleni kwake. "Karibu shemeji huku ndiko nakoishi siku hizi.

Wakati wanazungumza. Akili ya Kamal iliendа mbali sana. Alimkumbuka Mariamu mpenzi wake. Siku zote wakati yupo hai alikuwa akiwaambia kuwa wamefanana sana kama mapacha. Lakini kumbe ni mtoto wa mama mkubwa na mdogo. Teddy alijua hilo. Kwa sababu kuna wakati wanazungumza, halafu anamwangalia usoni mpaka akajisahau. Anakuwa hazungumzi tena mpaka Teddy anapomshtua. Wote wawili wakakumbuka mazungumzo ya zamani waliokuwa wakizungumza wakati Kamal mwenyewe alipokuwa akiwachukua mpenzi wake Mariamu na Teddy kwenda kula chakula cha jioni, au kuwatoa auti.

Kamal alikuwa anapenda mno kumtania. Alimwita mke mdogo. Mariamu alizaliwa na mkubwa, Teddy mdogo, ambapo mama zao walizaliwa tumbo moja.

Kamal alimzoea zaidi Teddy kuliko ndugu wengine. "Yaani mmefanana na dada yako kama korosho." Kamal alikuwa akimtania Teddy.


"Ikitokea bahati mbaya nikifa, muoe Teddy, mimi nitakuwa radhi kabisa, lakini ukioa mwanamke mwingine nitakutokea usiku wewe na huyo mkeo." Ni maneno aliyokuwa akiyaongea Mariamu mara kwa mara, anapokuwa na Kamal pamoja na Teddy.

Hakuna aliyekuwa akiyatilia maanani kwa sababu yalionekana ni kama maneno ya utani na kunogesha stori.

"Dada aliyekwambia wewe utaanza kufa kabla ya mimi nani? Ushaanza hivyo, hapa tuko kwenye furaha unaanza mambo yako." Teddy huwa wanajibu.

"Nasema ikitokea, sisi binadamu, huoni tulivyofanana, Kamal akiwa na wewe ataona kama yupo na mimi tu." Mariamu aliendelea.

"Teddy, achana na dada yako, anatuvuruga tu hapa, ukianza kuolewa kabla yeye hajafa halafu baadaye akifa na wewe upo kwenye ndoa, nitaachanisha ili nimuoe?"




**"Dada nimefanya hivi kwa sababu hata wewe ulipokuwa hai uliwahi kusema hili kuwa ungependa mimi niwe na Kamal kama ukitangulia kufa. Japo ulionekana kama mzaha lakini kweli imetokea na mimi sitaki kumpoteza aende kwingine. Atabaki kwenye ukoo wetu." Akamaliza Teddy.**

Hayo ni maongezi ya mara kwa mara ambayo huongelewa pale, Kamal anapokuwa pamoja na ndugu hao wawili, Mariamu na Teddy, ambapo huwachukua na kwenda nao kula bata, mwenyewe aliwaita wake zake, Mariamu mkubwa, Teddy mdogo.

"Ndiyo nimekuja hivyo!" Akasema Kamal kwa bashasha. "Umekuja kufanya nini?" Akauliza Teddy. "Unajifanya hujui eee!" Ni kama Teddy alionekana kufanya mzaha. "Kutimiza ahadi niliyokuahidi!" "Ipi?" "Ya kutaka kukuoa!" Akajibu Kamal na kusababisha kicheko cha kimbea kutoka kwa Teddy. Hakujibu kitu. Akabaki anatabasamu. "Kwanza ndugu zako wamenisamehe?" Akauliza tena. "Kwani umefanya nini?" "Walionekana kutonipenda baada ya kusikia mimi ndiye niliyemuua ndugu yenu Mariamu!" "Mhh.. mbona limewashuka shu! Mimi ndiye nimekuwa mshindi. Wakati umetoroka, walikuwa wananisakama kuwa inawezekana hata mimi nimeshirikiana na wewe kumuua, kwa sababu kwanza unaonekana kunipenda sana, halafu nakutetea sana. Sasa ulipojitokeza ukiwa umefanya upelelezi wako na yule mwenzako polisi, na mahakama ikathibitisha, kila mtu alibaki mdomo wazi. Wao sasa ndiyo wamenituma kwako uwasamehe kwa kukufikiria vibaya." "Okay, mimi sina tatizo na hilo, kwa sababu walikuwa wana uchungu na ndugu yao, sawa, lakini kwa sababu wameshapata ukweli na wamejirudi sawa, ila mimi nitawasamehe zaidi kama watakubali ombi la kutaka kukuchumbia wewe." "Omba lingine kaka, ilivyotoka taarifa ya Materu kukamatwa na kesi kuwa mahakamani, kabla hata ya hukumu, tulikaa kikao na kila mtu alikuzungumzia wewe, kila mmoja alisema kumbe ni mtu nzuri sana na umeweza kufichua mambo mabaya yaliyofanyika kwa dada yangu. Ndugu wengine wakasema kabisa nikutafute ili kama unahitaji kunioa unioe badala ya Mariamu ili wasikupoteze." "Kumbe eee!" Alisema Kamal na kusababisha Teddy aangue kicheko.

************************************

Wiki moja baadaye kila kitu kilikuwa kimekamilika. Tayari Kamal alikuwa ameshapeleka barua ya uchumba kama ile aliyopeleka kwa Mariamu na ikakubaliwa na ndugu. Yule yule aliyetaka kumuoa Mariamu, sasa amemchumbia Teddy, mdogo wake kwa mama mkubwa na mdogo.

Kila mmoja aliridhia kwa sababu hawakutaka kumpoteza Kamal. Kikubwa aliwaambia baada ya kutoa barua hiyo, anatakiwa kwenda kwenye mafunzo ya upolisi kwa miezi mitatu, akirejea ndiyo watafunga ndoa. Ikakubaliwa.

"Unajua Teddy, baada ya ndoa nikitoka Moshi, nitakaa uraiani kwa miezi mitatu mingine halafu nikakwenda nje ya nchi kwa mafunzo mengine maalum ya kijeshi."

Hakutaka kumwambia moja kwa moja kuwa atakwenda nchini Urusi kwa mafunzo ya sanaa za mapigano na upelelezi, kwani polisi walivutiwa na ushiriki wake katika kisa cha Materu.

Tayari Kamal na Teddy wakawa si wapenzi rasmi, lakini ni wachumba rasmi. Wakaanza kufuatana kokote wanakokwenda, ingawa kila mmoja alikuwa na kwake. Waliamua tu siku wake Chang'ombe kwa Teddy, au kwa Kamal.

Siku moja waliitenga kwenda kwenye kaburi la Mariamu. Walipofika walipiga magoti na kuanza kusali.

"Dada nimefanya hivi kwa sababu hata wewe ulipokuwa hai uliwahi kusema hili kuwa ungependa mimi niwe na Kamal kama ukitangulia kufa. Japo ulionekana kama mzaha lakini kweli imetokea na mimi sitaki kumpoteza aende kwingine. Atabaki kwenye ukoo wetu." Akamaliza Teddy.

"Sasa lala kwa amani mpenzi wangu Mariamu. Nimelipa kisasi kwa wote waliodhulumu roho yako. Niliapa sitosinzia wala kulala kama wauaji bado watakuwa hawajapatikana na kupatya hukumu inayostahili. Nimepambana nimewapata na kila aliyehusika amepata stahiki yake. Tukio nililolifanya limenifanya nionekane shujaa kwa wananchi na taifa. Nimepata kazi kwenye Jeshi la Polisi na baadaye nikakuwa askari mkubwa sana. Nataka kurudisha heshima kwenye ukoo wenu. Sitaki kwenda mbali, nimemchukua mdogo wako Teddy ambaye tulimpenda mimi na wewe, na ulisema ikitokea la kutokea huyu awe mbadala wako. Nitampenda na kumhudumia Teddy kama ulivyokuwa wewe. Mapenzi yetu kwako hayatotoka kwenye mioyo yetu. Lala salama Mariamu. Pumzika kwa amani. Damu yako haikupotea bure. Imeleta matokeo mengi chanya. Damu ya Mariamu." Akamaliza Kamal. Maombi ya Kamal yalimliza Teddy. Akachukua kitambaa na kumfuta machozi. Akamkumbatia. Akamshika mkono na kuanza kurejea taratibu kuelekea kwenye gari jipya ambalo Kamal alikuwa amenunuliwa na wananchi waliokunwa na kazi aliyoifanya.

**MWISHO**

# KOCHA AZAM ATAKA NYOTA WAPYA USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata mafanikio makubwa baada ya kukabidhiwa kikosi cha Azam FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rachid Taoussi, amewaambia mabosi wa timu hiyo anahitaji maboresho kwa kusajili wachezaji wapya kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema kocha huyo ametuma ripoti yake kwa uongozi ambayo inatarajiwa kufanyia kazi hivi karibuni.

**Pamoja na kwamba Ibwe hajasema ni wachezaji gani wanatakiwa kwenye ripoti hiyo, kocha huyo anahitaji wachezaji wapya kwenye baadhi ya maeneo ili kukiimarisha kikosi hicho ambacho kimemaliza mzunguko wa kwanza kikiwa na pointi 33.**

"Kocha tayari ametuma ripoti yake, kwa sasa menejimenti ipo kwenye kikao cha kuangalia mwalimu anataka nini, anataka wachezaji gani, sisi kama watendaji wengine tunasubiri ili tuone nini wataamua, nadhani ni kumwongezea wachezaji anaowahitaji kwa sababu tuna malengo makubwa sana msimu huu.

"Sisi malengo yetu msimu huu si kutengeneza tena kikosi, tuna wachezaji bora, kocha wa viwango vya juu na benchi zuri la ufundi, hakuna chochote tunachokihitaji zaidi ya ubingwa, hilo ni lengo mama na kama sivyo basi tutataka kuiona timu yetu ikishika nafasi ambayo itatupa tiketi ya kucheza michezo ya kimataifa msimu ujao, tunataka turudi kimataifa kwa sababu tunajua hivi tulivyo na kwa kiwango hiki tulichonacho tangu aje kocha Rachid Taoussi, tutafanya vizuri sana," alisema Ofisa Habari huyo.

Taoussi alikichukua kikosi cha Azam baada ya kutimuliwa aliyekuwa kocha kabla yake, Youssouph Dabo, alipotolewa katika raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho barani Afrika, dhidi ya APR ya Rwanda.

**WANIA...**



Wachezaji Yosso wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KenGold yatema watano, kugeukia walinzi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KenGold imetangaza kuachana na wachezaji wake watano, huku ikisema inataka kuongeza nguvu kwa kusajili watu wa eneo la ulinzi kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imewataja wachezaji waliopewa mkono wa kwaheri kuwa ni Steven Mganga, Amir Njeru, Castor Posta, Adam Uledi na Salum Idrissa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, wameamua kuachana na wachezaji hao ili kupata wengine ambao watakiongezea nguvu kikosi chao.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Omari Kapilima, mara kwa mara amekuwa akiilalamikia safu yake ya ulinzi kwa kutokuwa makini, akisema katika kipindi hiki cha usajili ni lazima aongeze nguvu.

"Tumemaliza mzunguko wa kwanza kwa kucheza mechi 15, bado michezo mingine 15, hivyo nafasi ya kubaki Ligi Kuu ipo kama tunafanya marekebisho kwenye safu yetu ya ulinzi kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

"Mabadiliko yatakuwa makubwa tu, siwezi kusema kama tutafumua kikosi ila kuna baadhi ya wachezaji wataondoka na kuwapisha wengine," alisema kocha huyo ambaye timu yake ilipata kipigo cha mabao 2-0 Jumatano ya wiki hii dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Mpaka inamaliza michezo yake ya mzunguko wa kwanza, KenGold inaburuza mkia, ikiwa imecheza mechi 15, ikishinda mmoja, sare tatu na kupoteza michezo 11, ikifunga mabao 10, ikiruhusu 27 kwenye wavu wake.

KenGold ni moja kati ya timu zilizopanda Ligi Kuu na kucheza kwa mara ya kwanza mwanzoni mwa msimu huu.

## Guede akaribia kutua Tabora Utd

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Singida Black Stars, imetangaza kuachana na straika Joseph Guede, raia wa Ivory Coast, huku taarifa zikieleza kuwa huenda akajiunga na Tabora United kwenda kuunganisha nguvu na wachezaji wa zamani wa Yanga, Heritier Makambo na Yacouba Songne.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imeeleza imeamua kuachana na mchezaji huyo kwa maslahi ya pande zote mbili, huku ikimtakia kila lakheri kwenye majukumu yake mapya.

"Tumefikia makubaliano ya pande mbili ya kuachana na aliyekuwa mchezaji wetu katika safu ya ushambuliaji, (Joseph Gnadou) Guede.

"Uongozi wa klabu unamshukuru kwa kipindi chote alichoitumikia timu yetu na tunamtakia kila la kheri katika safari yake ya soka," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Straika huyo alijiunga na Singida Black Stars mwanzoni mwa msimu huu na ameitumikia timu hiyo kwa kipindi cha miezi mitano tu, huku akiwa hana namba ya kudumu kikosini.

Kabla ya kujiunga na timu hiyo, Guede alikuwa akichezea Yanga, iliyomsajili kipindi cha dirisha dogo la usajili msimu uliopita na kuachwa mwishoni mwa msimu huo huo.

Hata hivyo, taarifa zinaeleza kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa mchezaji huyo kujiunga na Tabora United kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Habari zinasema mazungumzo baina ya pande zote mbili yanaendelea na yakikamilika anaweza kutangazwa kuwa mchezaji mpya, akiungana na wengine wa zamani wa Yanga, Makambo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Yacouba raia wa Burkina Faso.

Wakati huo huo, Klabu ya Namungo, imetangaza kusajili wachezaji wawili mpaka sasa kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili lililofunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imeeleza, wachezaji hao ni kiungo mshambuliaji, Najimu Mussa kutoka Singida Black Stars, huku ikimrejesha beki wa kati raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Derrick Mukombozi, ambaye aliachwa mwishoni mwa msimu uliopita.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**EDERSON AWANIWA UNITED**
KLABU ya Manchester United inamchunguza Ederson wa Atalanta mwenye umri wa miaka 25, na kiungo huyo wa kati wa Brazil ni mmoja wa wachezaji wachache ambao klabu hiyo inazingatia sana kumpata. (F***lorian Plettenberg***)

**FERGUSON ATAKIWA LEICESTER**
WEST Ham, Leicester City na Southampton zinaongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 20, kutoka Brighton. ***(Givemesport)***

**DIBLING ANUKIA KUUZWA**
KLABU ya Southampton inaweza kumuuza mchezaji wao chipukizi, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, ikiwa watashuka daraja kutoka Ligi Kuu, huku Manchester United na Newcastle United zikiwa na nia ya kumnunua kiungo huyo wa kati wa Uingereza. (***Football Insider)***

**POGBA NA MAN CITY**
UVUMI ulioenea kwamba, kiungo wa zamani wa Manchester United na Juventus, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 31, alikuwa ameonekana kwenye uwanja wa mazoezi wa Manchester City haukuwa wa kweli. (***Fabrizio Romano***)

**FAGIOLI AITAKA SPURS**
WEST Ham, Fulham na Crystal Palace zote zinamfuatilia kiungo wa Juventus, Nicolo Fagioli, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 23 anavutiwa na Tottenham Hotspur. (***Tuttosport)***

**SESKO ATAJWA CHELSEA**
CHELSEA inafikiria uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig na Slovenia, Benjamin Sesko, 21. (***TeamTalks***)

**HJULMAND KUPEWA MIKOBA**
BOSI wa West Brom, Carlos Corberan na kocha zamani wa Denmark, Kasper Hjulmand, ni miongoni mwa wanaowania kuchukua nafasi ya Russell Martin huko Southampton, lakini bosi wa muda, Simon Rusk, atabakia kuinoa kwa mchezo wa Jumapili ugenini dhidi ya Fulham. (***Sky Sports)***

**DUBRAVKA AWINDWA SAUDIA**
KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Shabab inavutiwa na dili la bei iliyopunguzwa kwa mlinda lango wa Newcastle United na Slovakia, Martin Dubravka, 35. (***I***)

**DANSO ALENGWA WOLVES**
KLABU ya Wolves inaweza kulenga uhamisho wa Januari kwa mlinzi wa kati wa Austria, Kevin Danso mwenye umri wa miaka 26, ambaye Lens inaweza kutaka kumuuza. ***(L'Equipe***)

**AKLIOUCHE AITAKA BARCA**
KIUNGO mshambuliaji wa Monaco na Ufaransa, Maghnes Akliouche mwenye umri wa miaka 22, amesema angependa kuichezea Barcelona katika maisha yake ya soka. ***(Sport)***

**NELSON KURUHUSIWA ARSENAL**
WINGA wa Arsenal, Reiss Nelson ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Fulham - ataruhusiwa kuondoka kwa 'Washikabunduki' hao msimu ujao kwa kuwa kuna uwezekano mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, hatokuwa sehemu kubwa ya mipango ya Mikel Arteta katika siku zijazo. ***(Mail Plus)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# STERLING HANA MPANGO WA KUONDOKA ARSENAL

**Licha ya ushiriki wake mdogo, anaendelea kujitolea katika klabu hiyo na kwa mujibu wa...**

**LONDON,** England

RAHEEM Sterling hana nia ya kuhitimisha mapema msimu wake wa mkopo wa muda mrefu pale Arsenal, kwa mujibu wa ripoti.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Liverpool na Manchester City, hakuwa chaguo la Enzo Maresca pale Stamford Bridge mwanzoni mwa msimu.

Akiwa ameachwa nje ya kikosi cha Chelsea kwa mechi ya kwanza ya Ligi Kuu England msimu huu, Sterling aliifungia siku yake ya mwisho kuichezea klabu hiyo.

**Kulikuwa na matumaini mengi kuhusu mpango huo wakati huo. Arsenal wanar ipotiwa kulipa chini ya nusu ya mshahara wa Ster ling wa pauni 325,000 kwa wiki - huku Chelsea wakilipa salio lililobaki.**

Hata hivyo, kuanza kwenye Ligi Kuu England imekuwa ngumu kwa Sterling na kuonekana kwa urefu wowote kumesimama katika wiki za hivi karibuni.

Bingwa huyo mara nne wa ligi ya juu ametazama kama mchezaji wa akiba ambaye hajatumika katika mechi nne za awali za Arsenal katika michuano yote.

Licha ya ushiriki wake mdogo, Sterling anaendelea kujitolea kwa Arsenal, kwa mujibu wa Evening Standard.

Fowadi huyo ameripotiwa kuwa bado amedhamiria kupambania namba katika kikosi cha Arsenal na bado anachukuliwa kuwa chaguo bora kwa Arteta.

# SLOT: CHIESA BADO HAJAWA SAWA




**LIVERPOOL,** England

ARNE Slot amewaambia mashabiki wa Liverpool kwamba, wasitegemee kumuona winga Federico Chiesa kuwa bora baada ya kurejea kutoka kwenye majeraha.

Chiesa aliyesajiliwa majira ya kiangazi aliingia akitokea benchi katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Southampton Jumatano na kufanya mechi yake ya nne tu msimu huu, akiwa amekaa nje ya uwanja kwa miezi mitatu iliyopita.

Lilikuwa ni onesho la mchanganyiko kutoka kwa Chiesa, lakini Slot alisisitiza kwamba hilo linatarajiwa kutoka kwa mchezaji ambaye bado anaongeza kasi.

"Sijui kama tuliona sawa, lakini nadhani nilichokiona ndicho unachoweza kutarajia," alisema Slot.

"Ikiwa mchezaji atakuwa nje kwa miezi mitano au sita, huwezi kutarajia mengi kutoka kwake.

"Niliona kupanda na kushuka. Niliona wakati mzuri sana na niliona wakati fulani ambapo nilihisi. Sawa, unaweza kufanya vizuri zaidi kuliko hii. Kwangu, hiyo ni kawaida kabisa ikiwa mchezaji amekuwa nje kwa muda mrefu na anacheza mchezo wake wa kwanza ndani ya miezi mitano au sita.

"Nilishasema hapo awali kwamba inaniwia vigumu sana kwa sababu kawaida katika maandalizi ya msimu mchezaji anapata mechi tatu, nne au tano hasa halafu anakuwa nje kwa wiki nne au tano tu.

"Badala yake, alikuwa nje kwa muda mrefu, kwa hiyo kumrudisha kwenye kiwango chake bora si rahisi, lakini ilikuwa nzuri kuona kwamba alionesha ubora fulani tayari."

# Barca yawaonya Araujo, de Jong



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeripotiwa kuwaonya beki wa kati Ronald Araujo na kiungo Frenkie de Jong kwamba watauzwa ikiwa hawatasaini mikataba mipya kabla ya mwisho wa msimu huu.

'La Blaugrana' hao wanakaribia kurejea kwenye sheria ya matumizi ya La Liga na uwezo wa kutumia euro bilioni moja iliyoongezwa - na sasa wanalenga kuwapa mikataba mipya wachezaji wao wa thamani zaidi.

Gavi na Pedri tayari wamekubali kuongeza mikataba yao ya muda mrefu, lakini kuna wasiwasi kwa Araujo na De Jong.

Wachezaji wote wawili wanakaribia kumaliza miezi 18 ya mwisho ya mikataba yao na Barcelona inasemekana kuweka wazi kuwa hawataruhusiwa kuingia mwaka wa mwisho wa mikataba yao.

Kwa hiyo, Araujo na De Jong wameonywa kwamba lazima watie saini mikataba mipya kabla ya Juni 30, 2025.

Kumekuwa na ishara tofauti linapokuja suala la mustakabali wa Araujo, huku ripoti moja hivi majuzi ikidai kulikuwa na hofu kwamba beki huyo anaweza kuondoka kwa uhamisho huru.

Araujo anajulikana kutaka kubakia Barcelona na ataongezewa mshahara iwapo ataamua kuongeza mkataba wake.

Kuhusu De Jong, kiungo huyo wa kati wa Uholanzi tayari ameruhusu ofa ya kuongeza muda.

# Amorim hajutii kumtoa Rashford

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesisitiza kuwa alikuwa sahihi kumtoa Marcus Rashford katika kikosi cha Manchester United licha ya kutolewa kwenye Kombe la Carabao katika hatua ya robo fainali kwa kichapo cha mabao 4-3 kutoka kwa Tottenham Hotspur juzi.

Rashford aliachwa nje ya kikosi cha Amorim kwa mechi ya pili mfululizo baada ya kuachwa kwenye ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Manchester City Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alipendekeza katika mahojiano ya Jumanne kwamba anataka kuondoka katika klabu hiyo.

Alipoulizwa baadaye kama kichapo cha Spurs kitamfanya afikirie upya msimamo wake kwa fowadi huyo wa England, Amorim alisema anasimamia uamuzi wake.

"Ninahisi kwamba ninafanya jambo sahihi kwa timu kwa hiyo si kosa," alisema kocha huyo.

"Lazima tufanye uteuzi. Nadhani halikuwa kosa kwa sababu siku zote ninafanya vema kwa ajili ya timu katika njia yangu ya kuona mambo."

Bila Rashford, United ilirejea kwa muda kutoka nyuma kwa mabao 3-0 na kufanya matokeo kuwa mabao 3-2 kutokana na makosa ya golikipa, Fraser Forster.

Spurs walifanya mabao kuwa 4-2 kabla ya Jonny Evans kufunga bao la tatu dakika za lala salama na vijana wa Ange Postecoglou kufanikiwa kutinga nusu fainali na sasa watacheza dhidi ya Liverpool.

Ulikuwa usiku mgumu kwa makipa wote wawili huku kipa namba mbili wa United, Altay Bayindir - alianza mbele ya Andre Onana na kutengeneza makosa ya mabao mawili.

Tottenham inawakaribisha Liverpool katika mechi yao ya nusu fainali ya kwanza wikendi ya Januari 6, mwakani, huku Newcastle United ikisafiri kumenyana na Arsenal huko Emirates.



## Ramovic atamba Yanga kuimarika

INATOKA UKURASA 24

Baada ya ushindi huo, Yanga imepanda kutoka nafasi ya nne hadi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi 30, nyuma ya Simba iliyo nafasi ya pili na pointi zake 31, huku Azam FC ikiwa kileleni na pointi zake 33.

Hata hivyo, Azam imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza, huku Simba na Yanga zikiwa zimecheza michezo 12 kila moja.

Katika mchezo wa juzi, ilipatikana 'hat-trick' ya kwanza kwenye Ligi Kuu, ikifungwa na straika Dube, aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu akitokea Azam.

Hadi anapata 'hat-trick' hiyo alikuwa hajafunga bao lolote kwenye ligi msimu huu, lakini alipachika mabao matatu, akiwa pia ni mchezaji bora wa mechi.

"Kilikuwa kipindi kigumu sana kwangu, lakini wanachama na mashabiki wa Yanga, viongozi na wachezaji walinionesha upendo, walinisapoti, kwa hiyo tuzo hii ya mchezaji bora pamoja na 'hat-trick' ni zawadi kwa Wanayanga wote, tumeshinda wote," alisema Dube.

Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah 'Bares' alilalamikia safu yake ya ulinzi kufanya makosa mengi na kusababisha kufungwa mabao rahisi.

"Niwapongeze Yanga wamepata ushindi, kikubwa ni kwamba tumefanya makosa ambayo wao wameyatumia.

"Kama unacheza na timu ambayo unajua mkikosea tu wachezaji wake wanaweza kukuadhibu, basi unabidi ujichunge sana, hatukufanya hivyo, tumeadhibiwa.

"Mfano tulikuwa tunatafuta bao la kusawazisha ili matokeo yawe 2-2, lakini tukafungwa bao la tatu rahisi sana, inavunja moyo hata kwa wale ambao wanapambana mbele kutafuta mabao, tumeruhusu mabao rahisi, hasa la tatu ni la kizembe sana, imeleta shida sana," alilalamika kocha huyo.

Baada ya kipigo hicho, Mashujaa inabaki na pointi zake 19, ikiwa imemaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya saba.

# KIPIGO KUTOKA KWA AZAM CHAISHTUA FOUNTAIN GATE

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Fountain Gate kimeanza mapema maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Namungo ili kuepuka kilichowatokea Desemba 17, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kwa kuchapwa mabao 2-0 na Azam FC.

Akuzungumza jana kutoka Babati mkoani Manyara, Ofisa Habari wa Fountain Gate, Issa Mbuzi, alisema mchezo wao dhidi ya Namungo unatarajiwa kupigwa Desemba 25, mwaka huu, ambapo itakuwa ni Sikukuu ya Krisimasi, kwenye Uwanja wa Tanzania Kwaraa, lakini wameanza kujiandaa mapema kwa sababu hawataki kitu kama kile kijirudie tena.

"Hatutaki kile kilichotupata kwenye Uwanja wa Azam Complex cha kufungwa mabao 2-0 na Azam FC kijirudie tena, tunafanya maandalizi makubwa ili kucheza na Namungo kwenye uwanja wetu na wa nyumbani, tunaimani na maandalizi ambayo tunaendelea nayo, tutapata ushindi na kuwafurahisha mashabiki wetu," alisema Mbuzi.

Ofisa Habari huyo alibainisha kuwa kikosi chao kilianza Ligi Kuu vema na kuna wakati kiliongoza ligi, lakini baadaye hali ilibadilika na kuanza kupoteza, akisema hali hiyo huwa inatokea kwenye mchezo wa soka.

Wakati Mbuzi akisema hayo, Kocha Mkuu, Mohamed Muya, alibainisha kuwa kipindi hiki cha dirisha dogo ataangalia zaidi kuimarisha upande wa ulinzi kwani unaonekana kuwa una matatizo.

Mmiliki wa klabu hiyo, Japhet Makau, amekiri kuwa na changamoto eneo la ulinzi na kuahidi kulifanyia marekebisho, huku akiisifu safu yake ya ushambuliaji kuwa ni moto wa kuotea mbali.

"Nadhani sisi ni moja kati ya timu iliyofunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu, changamoto ipo kwenye safu ya ulinzi, tutarekebisha hilo," alisema.

Fountain Gate imefunga mabao 23 mpaka sasa, ikishika nafasi ya pili kwa kufunga mabao mengi kwenye ligi nyuma ya Simba yenye mabao 24, lakini pia inakamata nafasi ya pili kwa kuruhusu mabao mengi, ikifanya hivyo mara 25, nyumba ya KenGold ambayo imeshabugizwa mabao 27 mpaka sasa.

Timu hiyo ina wachezaji wawili wanaofuatana kwa kusaka kiatu cha dhahabu ambao ni Selemani Mwalimu mwenye mabao sita, akiwa kwenye nafasi ya pili nyuma ya Elvis Rupia wa Singida Black Stars mwenye mabao saba, na Edgar William mwenye mabao matano.




Wachezaji vijana wakicheza mpira wa kikapu katika Uwanja wa Kituo cha Michezo Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMC yaita timu zinazotaka wachezaji kwa mkopo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC, imesema imekamilisha usajili wa kiungo mkabaji ambaye watamtangaza hivi karibuni kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii, ikitarajia pia kuongeza wachezaji wengine kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, na ikizikaribisha klabu zinazotaka wachezaji wao kwa mkopo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, alisema katika usajili ni lazima kuambatane na kuwatoa wachezaji, hivyo wanatarajia kuwatoa baadhi ya wachezaji kwenda klabu zingine kwa mkopo.

"Tumepokea ripoti fupi ya mwalimu kwa namna anavyohitaji kuwa na maboresho ya wachezaji kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, tunalifanyia kazi, tumeshafanya usajili wa mchezaji mmoja ambaye ni kiungo mkabaji, kwa sasa sitomtaja muda ukifika tutamtangaza kwenye kurasa rasmi za mtandao wa klabu yetu na yapo maingizo mengine ambayo tunatarajia kuongeza.

"Siku zote ukiongeza wachezaji basi ni lazima wengine waondoke, kuna ambao tunawapeleka sehemu nyingine kwa mkopo ili wapate muda wa kucheza zaidi, tunatarajia maombi kutoka klabu mbalimbali za Ligi Kuu au Championship zikihitaji wachezaji wetu, na tutawatangazia watakaoondoka," alisema Chukuchuku.

KMC imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza, ikiwa kwenye nafasi ya tisa, ikiwa na pointi 18 mpaka sasa.

Katika michezo hiyo 15, imeshinda mitano, sare tatu, ikipoteza mechi saba, ikifunga mabao 10 na kuruhusu 20 kwenye nyavu zake.

Wakati huo huo, kikosi cha timu hiyo kimerejea kambini jana Ijumaa kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa kwanza wa mzunguko wa pili, utakaochezwa Desemba 29, mwaka huu, dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Chukuchuku alisema baada ya mchezo wao dhidi ya Pamba Jiji, Jumatatu iliyopita, Kocha Mkuu Kalimangonga Ongalla, alitoa mapumziko ya muda mfupi.

"Leo (jana), kikosi chetu kinatarajia kuingia kambini kujiandaa na mchezo dhidi ya Coastal Union, tunaamini wana timu nzuri lakini tunakwenda kupambana kwa ajili ya kupata ushindi," alisema.

## *Mpanzu kuipaisha Simba Kagera leo?*

INATOKA UKURASA 24

leo, tunaona bora asicheze ili tumtumie kwenye mchezo unaofuata," alisema kocha huyo.

Alisema kuwa kutokana na kuwapo kwa michezo mingi iliyofuatana, amekuwa akikibadilisha kikosi chake mara kwa mara ili kila mchezaji asicheze michezo mingi na kusababisha kuchoka na kiwango kupungua.

"Ni muhimu sana kupumzisha wachezaji na kuwachezesha wengine, angalia mfululizo wa michezo yetu, tumecheza dhidi ya CS Sfaxien, siku mbili baadaye tumecheza dhidi ya KenGold, halafu tutacheza dhidi ya Kagera Sugar na baada ya hapa tunakwenda kucheza dhidi ya JKT Tanzania, hakuna mchezaji anayeweza kucheza dakika 90 michezo yote hii kwa kiwango kile kile," alifafanua kocha huyo.

Wakati huo huo, Katibu wa Chama cha Soka Mkoani Kagera, Al-Amin Abdul, amesema kikosi cha Kagera Sugar kilipata ajali wakati kikienda kwenye mkutano na waandishi wa habari kwa ajili ya mchezo wa leo.

Alisema katika kikosi hicho kulikuwa na Kocha Mkuu na wasaidizi wake, nahodha pamoja na wahusika wengine, ingawa hakujaripotiwa madhara makubwa.

"Tumefanya mkutano na timu moja tu ya Simba iliyofanikiwa kutokea, lakini timu wenyeji, Kagera Sugar, kwa masikitiko imepata ajali ikiwa njiani ikitoka klabuni ikija hapa, ilikuwa na Kocha Mkuu na wasaidizi wake, nahodha wa mchezo na wengine, kwa hiyo bado wapo sehemu ya tukio na tunaendelea kuwasiliana nao," alisema.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Desemba 21, 2024




Slot: Chiesa bado hajawa sawa UK. 22

KIWANGO...



Mshambuliaji wa Mashujaa FC, Ismail Mgunda, akijaribu kumhadaa beki wa kati wa Yanga, Dickson Job, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda mabao 3-2. **MPIGAPICHA WETU**

# MPANZU KUIPAISHA SIMBA KAGERA LEO?

## ●●● Kocha Fadlu atoa sababu kubadili kikosi chake huku akitaja watakaokosekana kuwa ni...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba leo kinatarajiwa kushuka kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera kucheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji, Kagera Sugar, huku macho na masikio ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo, yakitaka kushuhudia winga machachari, Elie Mpanzu, akishuka dimbani leo.

Wakati hayo yakiendelea, msafara wa makocha, nahodha wa Kagera Sugar ulipata ajali jana wakitoka klabuni kwenda kwenye mkutano wa waandishi wa habari kwa ajili ya mchezo huo.

Hata hivyo, taarifa zinaeleza kuwa wote waliokuwapo kwenye basi hilo la klabu wapo salama na walibaki kwenye eneo la ajali kwa ajili ya taratibu za kisheria.

Simba itaingia Uwanja wa Kaitaba ikiwa na kumbukumbu ya kutofanya vema uwanjani hapo kwenye michezo yake ya Ligi Kuu ikicheza na Kagera Sugar mara kadhaa.

Pamoja na rekodi kuwa si nzuri kwa Simba inapocheza uwanjani hapo, lakini wanachama na mashabiki wa timu hiyo wameonekana kuwa na matumaini kutokana na kuwa na uwezekano mkubwa wa kumuona kwa mara ya kwanza, Mpanzu, aliyesajiliwa miezi kadhaa iliyopita na timu hiyo akitokea Klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, lakini akitokea Klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji kwenye majaribio.

Awali, mchezaji huyo alitarajiwa kucheza kwenye mechi ya Jumatano iliyopita dhidi ya KenGold katika Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, lakini haikuwezekana kutokana na kuchelewa kupatikana Hati ya Uhamisho wa Kimataifa (ITC), pamoja na leseni inayomruhusu kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano ya Klabu hiyo, Ahmed Ally, kila kitu kilikamilika baadaye wakati mchezo unaendelea.

"Kuhusu Mpanzu, mambo yake yote yameshakamilika, iliyobaki ni kocha mwenyewe tu, Fadlu Davids, kama atamtumia, ila yuko tayari kuitumikia Simba, kwa maana hiyo wanachama na mashabiki wawe tayari kumuona mchezaji huyo akiitumikia timu kwa mara ya kwanza," alisema Ahmed.

Akizungumzia mechi hiyo, Kocha Mkuu, Fadlu alisema wapo tayari kwa mchezo huo, huku akisema kuna hatihati ya mchezaji wake Valentin Nouma kuukosa.

"Tuko tayari kwa mchezo, nimeiangalia Kagera Sugar ni timu nzuri kwa hiyo haitokuwa mechi rahisi, tutawaheshimu lakini tunataka tuitawale mechi na kuimaliza mapema.

"Tunaweza kumkosa Nouma aliumia kwenye mchezo uliopita, hajaumia sana, lakini yuko kwenye hatihati ya kutocheza

INAENDELEA UK. 23

## Ramovic atamba Yanga kuimarika

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Mashujaa FC iliyoupata juzi kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ametamba kuwa kikosi chake sasa kimeanza kuimarika, akiongeza kuwa siku kadhaa baadaye kitarudi kama kilivyokuwa huko nyuma, huku straika Prince Dube akifunguka kufunga 'hat-trick' ya kwanza katika Ligi Kuu.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Ramovic alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana kuhakikisha timu inapata ushindi katika mchezo mgumu uliokuwa na matukio ya kushangaza.

"Nawapongeza pia wapinzani wetu kwa kutupa mchezo mgumu, tulitawala sana kipindi cha kwanza, lakini mwisho wa mchezo mmeona ubao umesomeka mabao 3-2, ilikuwa ni mechi ngumu kama tulivyoitarajia, lakini kwa yote haya naona sasa kikosi kimeanza kuimarika taratibu ingawa bado hakijawa kwenye ubora unaotakiwa," alisema.

Kocha huyo alibainisha pamoja na kutawala dakika 45 za mwanzo, lakini walikuwa bora zaidi kwa dakika 25 tu ambapo walicheza kwa kasi kubwa kiasi cha kufanikiwa kufunga mabao mawili, baadaye wachezaji wake walionekana kukata pumzi kutokana na kutokuwa na utimamu wa mwili kwa asilimia 100.

"Nafikiri tulikuwa bora sana dakika 25 za mwanzo na tukafunga mabao mawili, baada ya hapo mnaweza kuona tulihangaika na tatizo kubwa ni utimamu wa mwili, tulishuka kwa sababu tulicheza kwa kasi kubwa mwanzo, tunahitaji tuendelee kujiboresha kwenye eneo hilo, ila nimefurahishwa mno na kiwango cha wachezaji wangu, ikizingatia kuna safari za mara kwa mara ambazo zinachosha wachezaji," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >